205.1

88 TU

Repmint 19

# TUPATE MAJI PAMOJA

**Integrated Fieldmanual**
**on**
**Community Participation**
**and Health Education**
**for**
**MAJI, AFYA and MAENDELEO**

205.1 88TU-3682

# TUPATE MAJI PAMOJA

**Integrated Fieldmanual**
**on**
**Community Participation**
**and Health Education**
**for**
**MAJI, AFYA and MAENDELEO**

RN: isn 3682
LO: 205.1 88TU

**First edition : January 1986**
**Second revised edition : December 1988**

## Hatua ya 1      Taarifa ya Kukubaliwa kwa Mradi wa Kijiji

Madhumuni

- Kukipa kijiji maelezo kuhusu maombi ya mradi wa kijiji.

Washiriki

Uongozi wa Wilaya ueleze vijiji vyote vilivyotuma maombi ya mradi wa maji uwezekano wa kutekelezwa kwa mradi au sababu za kushindwa kupatiwa mradi wa maji.

Maandalizi

- Ufafanuzi wa kanuni za utendaji.
- Uchambuzi wa maombi ya vijiji na nyaraka za mpango wa taifa wa maji.

Kazi itakayofanyika Kijijini

Hakuna

Hati

Barua za taarifa kwa vijiji vyote vinavyohusika.

Hatua ya 2 Uchunguzi

Mara inapoeleweka kuwa wataalam wa uchunguzi wataanza kuchunguza uwezekano na kutekeleza mradi wa maji, serikali ya kijiji kinachohusika ifahamishwe mapema.

Madhumuni

- Ili kuanza kwa mradi kueleweke kijijini.
- Kuijulisha serikali ya kijiji shughuli zitakazofanyika katika kijiji, taratibu na matatizo yanayoweza kujitokeza.
- Kuwashirikisha wanakijiji katika maamuzi ili kunufaika na ujuzi wao wa mazingira na pia kufahamu matakwa yao juu ya mradi wa maji.

Washiriki

Wataalam wa uchunguzi, uongozi wa kijiji na baadhi ya wanawake wa kijijini hapo.

Kazi zitakazofanyika Kijijini

- Wataalam wa uchunguzi kujulishwa kwa uongozi wa kijiji.
- Maelezo kwa uongozi wa kijiji kuhusu shughuli zitakazotekelezwa kijijini. Hizi ni pamoja na utekelezaji wa mradi wa maji wenyewe, usafi wa mazingira na matumizi ya maji kwa shughuli za uzalishaji.
- Kupatikana idhini ya kufanya uchunguzi toka kwa kijiji.
- Kutembelea kijiji pamoja na viongozi wa kijiji na baadhi ya wanawake ili kukusanya taarifa kuhusu:
  - . Wingi wa watu kijijini na ongezeko lao kwa mwaka.
  - . Matarajio ya kupanuka kwa kijiji.
  - . Vyanzo vya maji vilivyopo na utaratibu wa mgawanyo wa matumizi yake kati ya kunywa, kufua, kunyweshea bustani na mashamba n.k.
  - . Mahitaji ya ziada, k.m. sehemu za kufulia na za kunyweshea mifugo.
  - . Migongano inayoweza kutokea kati ya watumiaji wa maji (kwa mfano wafugaji na wanakijiji wengine).
  - . Idadi ya watu wenye uwezo wa kufanya kazi kijijini.
  - . Hali ya uongozi kijijini.
- Kuchimba visima vya majaribio au kuchunguza uwezekano wa kuwepo maji ya bomba.
- Kukutana na wanakijiji na kujadili nao matokeo ya uchunguzi. Baada ya majadiliano, wanakijiji waliohudhuria wanaombwa kuwajulisha wenzao matokeo ya uchunguzi.
- Kuwajulisha wanakijiji juu ya wakati mradi unapotegemewa kuanza kutekelezwa.
- Kuwapa wanakijiji habari zote muhimu juu ya utekelezaji wa mradi ili kuepusha hali ya wanakijiji kukosa imani. Mfano wa habari hizi ni sababu za kushindikana kuwepo kwa vituo vingi vya kuteka maji.

Hati

Ramani ya kijiji, ikionyesha makazi, vyanzo vya maji kijijini na umbali wake toka kijijini. Ielezwe pia kama vyanzo hivyo ni vya msimu au vya kudumu.

Mambo ya Kuzingatia

- Inabidi wanawake washirikishwe katika uchunguzi kutokana na ujuzi wao wa vyanzo vya maji na matumizi yake. Uongozi wa kijiji unaweza kumshirikisha mwanamke mmoja kutoka katika kila kitongoji kwenye uchunguzi.
- Kila inapowezekana, vituo vipya vya kuteka maji viwe karibu zaidi na watu kuliko vyanzo vya asili, ili kuwafanya watu watumie maji safi tu. Kama hili haliwezekani:
  - . Majadiliano yafanywe na wanavijiji juu ya kuvitengeneza vizuri vyanzo vya asili (ona Hatua ya 18B).
  - . Majadiliano yafanywe kati ya wanawake wa vitongoji vyenye maji safi na wa vitongoji visivyo na maji safi ili upatikane utaratibu mzuri wa kushirikiana maji safi yaliyopo. Uangaliwe pia uwezekano wa kuongeza visima au mabomba katika sehemu ambazo watu ni wengi, ili kupunguza misururu wakati wa kuteka maji.
  - . Pale ambapo kijiji chenye maji safi kinapakana na kijiji kisicho na maji, ufanywe utaratibu wa kushirikiana maji ili kuepusha matumizi mabaya ya maji au uharibifu.

Hatua ya 3A Kukusanya Taarifa Nyingine za Kijiji

Madhumuni

Kupata habari na taarifa kuhusu:

- Matatizo ya uongozi kijijini (kama yapo) na jinsi ya kuyatatua.
- Kutakiwa au kupendwa kwa mradi na wote au wengi wa wanakijiji wanaume na wanawake.
- Kazi za kujitolea na utaratibu wake kijijini.
- Mawasiliano sahihi yanayofaa kijijini.
- Uwezo wa kijiji kiuchumi ili kufahamu uwezekano wa matengenezo.

Washiriki

MAENDELEO, uongozi wa kijiji na baadhi ya wanawake wa kijijini.

Kazi zitakazofanyika Kijijini

- Kukusanya taarifa kuhusu idadi ya watu wenye uwezo wa kufanya kazi kijijini na utaratibu uliopo wa kufanya kazi (k.m. siku zilizopangwa kwa kazi za kujitolea).
- Kukusanya taarifa kuhusu mahitaji ya maji kwa matumizi mbalimbali, kama vile kunywa, kunywesha mifugo, umwagiliaji mashambani, kufyatua matofali, n.k.
- Kukusanya taarifa juu ya uwezekano wa wanakijiji kuchanga fedha kwa ajili ya matengenezo unapotokea uharibufu.
- Kuchunguza kama kuwepo kwa maji kijijini kutaokoa muda ambao wanawake walikuwa wanapoteza kufuata maji mbali, na kutafuta matumizi bora ya muda utakaookolewa.

Hati

Taarifa za uwezo wa kijiji kiuchumi, tabia za wanakijiji na shughuli za kimaendeleo zinazoweza kutekelezwa kijijini.

## Hatua ya 3B Kukusanya Taarifa Nyingine za Kijiji

**Madhumuni**

- Kupata picha kamili ya hali ya afya na usafi wa mazingira kijijini.
- Kuusaidia uongozi wa kijiji na wanavijiji kwa ujumla kuelewa uhusiano uliopo kati ya maji, usafi wa mazingira na afya.

**Washiriki**

AFYA, uongozi wa kijiji na baadhi ya wanawake kijijini.

**Kazi Zitakazofanyika Kijijini**

- Kukusanya taarifa zinazohusu idadi ya kaya zenye vyoo, sababu za kaya nyingine kutokuwa na vyoo, matumizi na usafi wa vyoo vilivyopo. Vitu vya kuangalia katika usafi ni usafi wa sakafu za vyoo, kuwepo kwa vifuniko vya mashimo ya vyoo, na kuwepo kwa maji na sabuni au majivu kwa ajili ya kunawa mikono. Mambo haya yatazamwe pia katika vyoo vya shule za msingi na zahanati.
- Kuangalia hali ya usafi katika vituo vya kuteka maji, sokoni, vituo vya mabasi n.k.
- Kuangalia tabia za utekaji maji na utunzaji wake majumbani. Mambo ya kuangalia hapa ni usafi wa vyombo, usafi wa mikono, usafi wa maji ya kunywa, desturi za kuchota maji ya kunywa (kutumia kata kwa kuchota badala ya chombo hicho hicho cha kunywea maji).

**Hati**

Taarifa za hali ya usafi kijijini na tabia za wanakijiji.

**Mambo ya Kuzingatia**

Uchunguzi wa dhati wa hali ya afya kijijini unaweza pia kufanyika kwa kushirikiana na kamati ndogo ya maji ya kijiji baada ya kuchaguliwa. Kwenye hali kama hii, uchunguzi wa awali kutakaokuwa umefanywa na AFYA utakuwa wa kijuu juu tu ili kutoa taarifa ya hali ya afya kwa mkutano wa kijiji.

Hatua ya 4A — Maandalizi ya Mkutano wa Kijiji juu ya Mradi

Madhumuni
- Kuusaidia uongozi wa kijiji kuandaa mkutano wa kijiji kwa namna ambayo wote au wengi wa watu wazima kijijini watahudhuria.
- Kuusaidia uongozi wa kijiji kuhakikisha kwamba wanawake wanahudhuria na kutoa mchango wao katika mkutano.
- Kusaidiana na serikali ya kijiji ili kupata taarifa muhimu za kijamii, kiuchumi, kiafya na ushirikishaji jamii katika mradi.

Washiriki
MAENDELEO na uongozi wa kijiji.

Kazi Zitakazofanyika Kijijini
Kujadili pamoja na uongozi wa kijiji muda, mahali na uendeshaji wa mkutano, na jinsi mahudhurio mazuri yatakavyohakikishwa.

Mambo ya Kuzingatia
Kati ya njia zitakazosaidia kuwafanya wanawake wahudhurie mikutano ni:
- Kufanya mkutano wakati na mahali panapowafaa wanawake.
- Kuwajulisha na kuwahimiza wanawake wahudhurie mikutano kwa kuutumia uongozi wa kijiji na vikundi vya wanawake. Namna ya kuwafanya watoe mchango wa mawazo katika mikutano ni pamoja na:
  - . Watu wote kuketi pamoja (kwa kuchanganyikana) badala ya wanaume kukaa mbele na wanawake kukaa nyuma yao.
  - . Wataalam (CDA, DFA na HA) kuwahimiza wanawake watoe mawazo.
  - . Matumizi ya lugha ya kienyeji ya mahali panapohusika pale inapowezekana. Wakati mwingine ni vema mtu anayefahamu lugha ya kienyeji atoe muhtasari wa yale yaliyozungumzwa kwa kiswahili.
  - . Kumwandaa na kumwalika msemaji wa kike ili aulize maswali na kutoa mawazo kwa niaba ya wanawake.

Baada ya mafunzo, mkufunzi anaweza kumwalika mmoja wa wakurufunzi kuongoza igizo la mkutano wa kijiji, wakati wakurufunzi wengine wakiwaigiza wanakijiji.

## Hatua ya 4B — Kukitaarifu Kijiji na Kujadili Kuhusu Mradi

### Madhumuni

- Kukielewesha kijiji mambo yafuatayo juu ya mradi:
  - . Muundo na usanii wa mradi, ambao utaelezwa na wataalam wa MAJI.
  - . Usafi wa mazingira ambao utaelezwa na AFYA.
  - . Kushirikishwa kwa wanakijiji katika hatua zote za mradi na matumizi bora ya maji kwa manufaa ya kijiji. Matumizi hayo ni pamoja na bustani za mboga, kufyatua matofali, vitalu vya miche ya matunda au miti, n.k. Haya yataelezwa na MAENDELEO.
- Kujibu maswali mbalimbali yatakayoulizwa na wanakijiji kuhusu mradi.
- Kujadili pamoja na wanakijiji na kukubaliana juu ya vituo vilivyoonekana vinafaa kitaalam vya kutekea maji.
- Kujadili pamoja na wanakijiji huduma za ziada zitakazotakiwa, kwa mfano sehemu za kufulia, sehemu za kunyweshea mifugo, n.k., na kuangalia uwezekano wa kijiji kugharamia huduma hizo.
- Kuweka wazi vipengele vitakavyosababisha kubadilishwa kwa sehemu za kujenga visima au kuweka mabomba.
- Kufanya uchaguzi wa Kamati Ndogo ya Maji ya Kijiji (VWSC).
- Kuweka sahihi makubaliano ya kutekeleza mradi.

### Washiriki

Wanakijiji watu wazima wote, MAJI, AFYA, MAENDELEO na watumishi wengine wa serikali walioko kijijini, kama waalimu, watumishi wa KILIMO, MALIASILI, n.k.

### Kazi Zitakazofanyika Kijijini

- MAJI, AFYA na MAENDELEO watakijulisha kijiji hatua iliyofikiwa katika matayarisho ya mradi.
- MAENDELEO watausomea mkutano makubaliano ya kutekeleza mradi.
- Majadiliano juu ya hatua iliyofikiwa na makubaliano ya utekelezaji.
- Kama kuna vipengele ambavyo makubaliano hayajafikiwa, MAENDELEO watavisoma, ili vijadiliwe na makubaliano kufikiwa.
- MAENDELEO watausomea mkutano mabadiliko yatakayokuwa yamefanywa, kisha mwenyekiti wa kijiji atatia sahihi makubaliano ya utekelezaji wa mradi kwa niaba ya wanakijiji wote.
- Kamati Ndogo ya Maji ya Kijiji (VWSC) itachaguliwa.
- Kama upo umuhimu, uchunguzi wa ziada utafanywa.

### Hati

Makubaliano yaliyotiwa sahihi na ramani ya Kijiji ikionyesha usanii wa mradi.

### Jambo la Kuzingatia

Kama inakuwa vigumu kufikia makubaliano, kijiji kipewe muda zaidi, na ikibidi hatua ya 4B irudiwe.

<u>Kumbuka</u>

- Kamati Ndogo ya Maji ya Kijiji itakuwa na wajumbe wafuatao:
  . Mwenyekiti atakuwa ni yule mwenyekiti wa kamati ya Elimu, Utamaduni na Ustawi wa Jamii.
  . Mjumbe mmoja kutoka Kamati ya Ujenzi.
  . Wajumbe watatu wa kuchaguliwa.
  . Wajumbe wasiopungua wawili watakuwa wanawake.
- Kuunda kamati Ndogo ya Maji ya kijiji, mambo yafuatayo yajadiliwe na serikali ya kijiji. Hata hivyo haya ni mapendekezo tu, uamuzi wa mwisho ni wa kijiji chenyewe.
  . Jina: Kamati Ndogo ya Maji ya Kijiji.
  . Maskani: Jina la Kijiji, Kata, Wilaya na Mkoa
  . Madhumuni: k.m. kuhakikisha upatikanaji wa maji wakati wote na kuongeza matumizi bora ya maji.
  . Tarehe ya kundwa.
  . Kutambulika kisheria: Kama vile kupitishwa na vikao vinavyohusika vya kijiji.
  . Wajumbe: Ona hapo juu (kumbuka)
  . Uwakilishi: k.m. Angalau mwenyekiti na katibu wawepo, na mjumbe mmoja.
  . Kazi: K.m. Kushiriki katika mipango na usanii.
    Kuandaa watu kwa kazi za kujitolea katika ujenzi.
    Kufuatilia upatikanaji wa maji wakati wote.
    Kupanga na kutekeleza mipango ya afya kijijini.
    Kupanga na kutekeleza shughuli za maendeleo.
    yatokanayo na maji, k.m. bustani, kufyatua matofali n.k.
  . Uchaguzi wa wajumbe: Muda - baada tu ya mradi kuanza
    kipindi - k.m. miaka mitano.
    uwezekano wa kuchaguliwa zaidi ya mara moja.
  . Taratibu za kuomba kuitishwa kwa mkutano mkuu wa kijiji.
  . Wajibu wa VWSC mbele ya mkutano mkuu:
    Taarifa ya kipindi kilichopita
    Kuratibu uchaguzi wa kamati ya kudhibiti fedha
    Kuratibu uchaguzi wa VWSC mpya
    Mambo mengineyo muhimu.
  . Taratibu za kubadili katiba ya VWSC.

Ni vema kama katika hatua hii majadiliano yataanza kuhusu michango kwa ajili ya matengenezo na gharama nyingine za mradi (ona hatua za 6 na 10).

## Hatua ya 5A Kuwaandaa Watu kwa Kazi za Kujitolea

**Madhumuni**
- Kujiandaa kuanza ujenzi wa mradi.

**Washiriki**
MAENDELEO na Kamati Ndogo ya Maji ya Kijiji.

**Kazi Zitakazofanyika Kijijini**
- MAENDELEO watawasaidia Kamati Ndogo ya Maji ya Kijiji kuorodhesha watu wote wenye uwezo wa kufanya kazi kijijini na kuwagawa katika vikundi vya kufanya kazi.
- MAENDELEO na MAJI watasaidia kuvipangia vikundi mbalimbali kazi ama kwa vipimo au kwa siku maalum.
- MAENDELEO watawasaidia Kamati Ndogo ya Maji ya Kijiji kuweka orodha ya mahudhurio katika kazi.
- MAENDELEO na MAJI watafuatilia utendaji, na kuingilia kati kuisaidia VWSC kama mahudhurio yatashuka.
- Kijiji kitatoa mchango kwa ajili ya kazi zote zisizo za kuchagua fedha za kuwalipa vibarua.
- MAJI watawajulisha VWSC na MAENDELEO mpango wa kazi. Ujulisho huo utafanyika siku za Ijumaa, Jumamosi au Jumapili inayotangulia siku ya kuanza ujenzi.
  Uchaguzi wa siku utategemea watu wengi ni wa dini au dhehebu gani
  . siku ambazo watu wengi hawako kazini.

**Hati**
- Orodha ya watu wote wenye uwezo wa kufanya kazi kijijini ambayo itatunzwa na VWSC.
- Orodha ya mahudhurio ya kila siku.
- Mpango wa kazi ya ujenzi.

**Mambo ya Kuzingatia**
Kama wanakijiji hawawezi kushiriki kufanya kazi kwa sababu moja au nyingine, itabidi wachange fedha ili vibarua waajiriwe. Wakati wowote ule, watu wa kujitolea wasilipwe kwa fedha za mradi, ingawaje utaratibu huo upo katika baadhi ya miradi. Ili kupanga kazi, jadiliana na VWSC juu ya njia zinazofaa za kuwahamasisha watu, kulingana na mazingira ya kijiji.
Njia moja inayowezekana ni kwa DFA wataandika orodha ya watu wenye duwezo wa kufanya kazi kijijini, watagawa kazi na kuweka korodha ya mahudhurio. Njia ya pili ingeweza kuwa kuandika orodha ya watu watakaofanya kazi za kujitolea katika kila siku moja ya juma. Uzuri wa njia hii ni kwamba hupunguza tabia ya kutegeana.

Mambo yafuatayo yatahitaji kuangaliwa kwa undani zaidi wakati wa kupanga kazi:

- Kuepuka kupanga kazi za kujitolea wakati wa shughuli nyingi, k.m. msimu wa kilimo.
- Mgawanyo wa kazi kwa haki, ikiwa ni pamoja na kati ya wanawake na wanaume.
- Kuepuka kuwa na kundi kubwa la watu kazini siku za mwanzo, kwa sababu kwanza usimamizi utakuwa mgumu na pili idadi hiyo kubwa haitaweza kudumishwa.

Mara nyingi, hamasa ya kazi hupungua kadri muda unavyopita. Njia za kufufua hamasa ni pamoja na:

- Kuitisha mkutano wa wanakijiji kuzungumzia mradi. Wanawake watumiwe katika kuhamasisha watu wahudhurie.
- Kupanga kazi upya, na kwa miradi ya maji ya bomba, kuanza kulaza mabomba katika sehemu ya mtaro iliyokamilika.
- VWSC itoe vibali kwa watu wenye udhuru wa kutoshiriki katika kazi, k.m. muuza duka.

Sababu kubwa ambayo hufanya hamasa ya kazi ishuke, ni ahadi za serikali kuu au mhisani wa mradi kutotimizwa. Hali kama hiyo inapokuwa imejitokeza, ni vigumu sana kuwahamasisha upya watu washiriki katika utekelezaji wa mradi.

<u>Kumbuka</u>
Wakati wa hatua hii, majadiliano yanaweza kuanza kuhusu uteuzi wa VM/VSA ambao utafanywa na VWSC.

## Hatua ya 5B — Elimu juu ya Viwango vya kazi na Ufuatiliaji wake

Madhumuni
- VWSC iweze kuelewa umuhimu wa viwango vya kazi vinavyohitajika ili maji yapatikane wakati wote.
- VWSC iweze kueleza na kuonyesha kwa vitendo viwango vya kazi wakati wa kazi za kujitolea.
- VWSC iweze kusimamia kazi za kujitolea kufuatana na viwango vinavyostahili.

Washiriki
- MAJI, MAENDELEO, VWSC na watu watakaoshiriki katika kazi za kujitolea.

Kazi Zitakazofanyika Kijijini
- MAJI na MAENDELEO watawasaidia VWSC katika kuonyesha namna ya kuchimba mtaro.
- MAJI na MAENDELEO watawasaidia VWSC jinsi ya kusimamia kazi iwe nzuri.

Jinsi ya Kuonyesha Viwango vya Kazi
- Tafuta vifaa vinavyotakiwa:
  - . Vipande vya bomba la mpira vilivyochomwa sana na jua
  - . Vipande vya bomba ya plastiki ambayo ni rahisi kuvunjika na vilivyotobolewa.
  - . Kibiriti cha chuma.
  - . Kamba
  - . Kijiti cha kupimia.
  - . Jembe.
- Itisha mkutano wa watu wote watakaoshiriki katika kazi za kujitolea.
- Onyesha uchimbaji wa mtaro wenye kina kufupi.
- Waambie wanakijiji wafikirie juu ya hadidhi inayofuata:

"Kijiji kimekuwa kikichimba mitaro yenye vina vifupi kwa ajili ya bomba lao la maji. Wakati wa mvua maji mengi yanatiririka kwenye mitelemko. Mabomba yanapatwa na nini?" (Jibu litolewe na washiriki).

"Sasa wakati wa kiangazi jua linawaka sana na mionzi ya jua inayapiga mabomba haya. Kunatokea nini?"

(Maelezo yatolewe na MAJI, kama jibu halijulikani).
(Kuwe na kielelezo cha kuvunja bomba la plastiki ambalo ni jepesi kuvunjika na mmoja wa washiriki).

"Pia kuna moto wa maporini. Nini kinatokea kwa bomba?"
(Kielelezo cha bomba la plastiki likiyeyuka).
"Chini ya mtaro jiwe lenye ncha kali limeachwa. Kunatokea nini?"
(Onyesha kipande cha bomba kilichotoboka).

"Uzuri wa kazi unaweza kuimarishwa na kuongezwa vipi?"
(Maelezo juu ya utumiaji wa kamba na kijiti cha kipimo maalum katika kuchimba mitaro).

Uamuzi wa Pamoja
Ni muhimu kwamba mitaro ichimbwe kwa kunyooka, kwa kina cha kutosha, chini panalainishwa inavyotakiwa na baada ya kutandika bomba, mitaro inafukiwa vizuri ili bomba letu lisivunjike kirahisi.

Hatua ya 6A — Uteuzi wa malipo ya VM/VSA

Madhumuni
- Kuteua watu wanaofaa kuwa VM na VSA toka kati ya watu waliokuwa wanafanya kazi za kujitolea.
- Kuwasaidia VWSC kupanga utaratibu wa malipo ya VM na VSA.

Washiriki
MAJI, MAENDELEO na VWSC.

Kazi Zitakazofanyika Kijijini
- Kueleza kazi za VM na VSA na kuandaa utaratibu wa mafunzo yao.
- Kujadili aina ya watu watakaofaa kuwa VM/VSA
- Kuitaka VWSC ichague watu watakaohudhuria mafunzo.
- Kuanzisha mafunzo ya kazini kwa ajili ya wateuliwa.
- Kujadili ni vipi VWSC itawalipa VM/VSA na watalipwa kiasi gani.
- Baada ya mradi kukamilika, MAJI watatoa mafunzo ya rejea kwa VM/VSA wakati wa ziara vijijini. Pia MAJI watatoa mafunzo kwa VM/VSA wapya pale inapobidi.

Mambo ya Kukumbuka
Kazi za VM/VSA:
- Huduma nzuri kwa wanakijiji
- Mawasiliano na VWSC
- Usimamizi wa VCT's
- Matengenezo ya sehemu mbalimbali za visima au vyanzo vya maji ya mabomba.
- Kuishauri VWSC juu ya mambo yote yanahusu mradi - matengenezo, uendeshaji, matumizi ya maji kwa uzalishaji, n.k.
- Ununuzi wa vipuli na vifaa kwa ajili ya matengenezo ya mradi, au kuvipata toka kwa DFA au mgawaji mwingine.
- Katika uteuzi wa watu watakaofunzwa kuwa VM/VSA, mambo yafuatayo ni ya kuzingatia:
  . Wawe ni wakazi wa kudumu kijijini.
  . Watu wanaotambua wajibu wao na wa kuaminika.
  . Wawe ni watu wenye uwezo wa kufanya kila kazi iliyoorodheshwa.
  . Wawe ni watu wanaopenda kazi.
- Majadiliano yafanywe na wanakijiji juu ya uwezekano wa kuwachagua wanawake, kutokana na hamu yao binafsi ya kupatikana maji kwa matumizi ya nyumbani bila matatizo. Kwa vile wanaume mara nyingi hufanya kazi nje ya kijiji, huduma zao kwa upande wa maji zinaweza zisiwe za kutegemewa sana.
- Kwa upande mwingine, kama mtu mwaminifu na mwenye uwezo akichaguliwa, fikiria uwezekano wa kuwapeleka mume na mke kwa mafunzo, ili kama mmoja hayupo mwingine aweze kufanya kazi zake. Kwa njia hii, watu wawili watafanya kazi kwa mshahara mmoja, na mke atapata mafunzo kamili na sahihi, kutoka kwa mwalimu.

- Mambo ya kufikiria katika malipo ni:
  . Malipo kulingana na kazi iliyofanywa.
  . Kutokushiriki katika kazi nyingine za pamoja kijijini bila kupoteza sehemu yake ya manufaa.
- Inapendekezwa kwamba kwa miradi ya maji ya bomba yanayosukumwa kwa mashine, mwangalizi wa pampu akae karibu na 'pumphouse' ili kuzuia wizi wa sehemu za pampu.

Hati
Orodha ya kazi za VM/VSA.

Hatua ya 6B Uteuzi na Malipo ya VCT

MADHUMUNI
- Kuteua watu wanaofaa kuwa waangalizi wa vituo vya maji kijijini.
- Kuwasaidia VWSC kupanga utaratibu wa motisha kwa VCT.

Washiriki
MAENDELEO na VWSC

Kazi zitakazofanyika Kijijini
- MAENDELEO na VWSC kwa pamoja watafikiria kazi za VCT.
- VWSC watatafuta watu wanaofaa kwa kazi hiyo.

Mambo ya Kukumbuka
- Kazi za VCT ni:
  . Kuhakikisha hali ya usafi kwenye mazingira ya kituo cha maji
  . Kuwaelimisha watumiaji maji juu ya umuhimu wa usafi katika mazingira ya kituo cha maji na matumizi bora ya maji nyumbani.
  . Kutoa taarifa ya matatizo yoyote ya pampu au bomba kwa VM/VSA na VWSC.
- Mambo ya Kuzingatia katika Kuwateua VCT'S:
  . Wawe wanaishi karibu na vituo vya maji.
  . Wawe ni wakazi wa kudumu kijijini.
  . Watu wanaotambua wajibu wao na wa kuaminika.
  . Watu wenye uwezo wa kuzungumza vizuri na watu wengine.
  . Watu wanaopenda kazi zao.
  . Watakaokubali kufanya kila kazi pamoja na kufanya usafi.
- Inapendekezwa kwamba kila inapowezekana wanawake wachaguliwe kwa kazi hiyo kwa sababu:
  . Wanawake huenda mara kwa mara kwenye vituo vya maji.
  . Wanawake wana shauku ya kuona kwamba maji yanapatikana wakati wote.
  . Wanawake hawasafiri safiri mara nyingi nje ya kijiji.

Pale ambapo VCT mwanamke atashindwa kutekeleza shughuli zake, atasaidiwa na mjumbe wake wa nyumba kumi na VWSC.

- Motisha ya VCT:
  Njia za kuwapa motisha VCT ni pamoja na:
  . Kuwa wa haki ya kulima bustani karibu na kituo cha maji (pale ambapo kipo kwenye eneo la jumuiya).
  . Kupewa udhuru wa kutofanya kazi nyingine za kujitolea kijijini.

Hatua ya 7 Ujenzi wa Huduma za Ziada

Madhumuni
- Kurahisisha matumizi ya maji kwa ajili ya usafi wa mwili, mavazi na uzalishaji bila kuchafua mazingira ya kituo cha maji.
- Kuwapunguzia wanawake taabu ya kubeba maji kupeleka nyumbani kwa ajili ya kufulia na kuogesha watoto.
- Kupunguza migogoro kati ya jamii tofauti, k.m. wakulima na wafugaji.
- Kuongeza pato la kijiji na kuongeza upatikanaji wa vyakula muhimu kwa afya za wanakijiji.

Washiriki
MAJI, MAENDELEO, AFYA, VWSC na wanakijiji.

Kazi Zitakazofanyika Kijijini
- MAJI watachunguza uwezekano wa kujengwa kwa huduma za ziada kama vile sehemu za kufulia na kuoga, sehemu ya kunyweshea mifugo, mifereji ya umwagiliaji, mabwawa ya samaki, n.k. na kuwajulisha wanakijiji.
- MAENDELEO, AFYA na VWSC watawaelimisha wanakijiji juu ya manufaa ya matumizi bora ya huduma za ziada zitakazokuwepo.
- Wanakijiji watashiriki kwa kujitolea kufanya kazi na michango kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vitakavyohitajika.
- Baada ya ujenzi wa huduma hizo kukamilika, VCT na VWSC watalihakikisha kuwa zinatumiwa kama ipasavyo na kutunzwa.
- Itabidi wanakijiji watoe mawazo yao juu ya ujenzi wa huduma za ziada, kwa mfano wanawake wataeleza aina ya sehemu za kufulia wanazopendelea na wanaume wataeleza aina za karo za kunyweshea mifugo watakazopendelea.

Mambo ya Kuzingatia
- Kuna baadhi yahuduma za ziada ambazo kabla ujenzi wake haujatekelezwa itabidi yawepo mawasiliano na idara nyingine. Kwa mfano kabla ya kuchimba bwawa la samaki itabidi MALIASILI wajulishwe na watoe mchango wao wa kitaalam juu ya mradi huo.
- Kwa vile uoshaji wa vyombo utachafua mazingira ya kituo cha maji, iwe ni marufuku kuoshea vyombo kwenye kituo cha maji. Hata hivyo, kama kuna bwawa la samaki, vyombo vinaweza kuoshwa na mabaki ya chakula kutupwa kwenye bwawa.
- Mtu yeyote atakayetumia maji kwa ajili ya shughuli za uzalishaji wake binafsi, km. kufyatua matofali, itabidi atoe mchango mkubwa zaidi kwa ajili ya mfuko wa maji kijijini.

Hatua ya 8A — Elimu ya Afya: Uchunguzi wa Hali ya Usafi Kijijini

Madhumuni
- Kuona hali ya usafi kijijini na kubuni njia za kurekebisha hali ili mradi wa maji ulete manufaa ya afya kwa jamii.
- Kutengeneza mpango wa kutekeleza marekebisho ya hali ya usafi kijijini.

Washiriki
AFYA na VWSC

Kazi Zitakazofanyika Kijijini
- Kwa kupitia kwa VWSC, wanakijiji waombwe ruhusa ya kutembelea kijiji chao ili kuchunguza hali ya usafi.
- Kwa kusaidiana na VWSC, AFYA watatembelea kaya zote kijijini kuona hali ya usafi. Endapo kijiji ni kikubwa sana, kaya kadhaa katika kila nyumba kumi, zinaweza kutembelewa.
- Kueleza madhumuni ya matembezi yatakayofanywa, na kupata kibali cha kuona vyoo na vyombo vya kutunzia maji ya kunywa.

Mambo ya Kuangalia
- Kuwepo kwa choo
- Kama hakipo, sababu ya kutokuwepo
- Kama kipo, hali yake:

| | |
|---|---|
| . Kibanda | kizuri/wastani/kibaya |
| . Sakafu | nzuri/wastani/mbaya |
| . Kifuniko cha shimo | kipo/kipo pembeni/hakipo |
| . Maji na sabuni au jivu la kunawia | vipo/havipo |

- Omba ruhusa ya kuona jinsi maji ya kunywa yanavyotunzwa
  - . Kuna mahali maalum yanapotunzwa
  - . Yamefunikwa
  - . Kikombe/chombo maalum cha kunywea maji kwa kila mtu
  - . Kata au chombo maalum cha kuchota maji toka kwenye mtungi au ndoo
- Maji ya kunywa yanapatikana wapi?
  - . Pampu ya mkono, sababu .................
  - . Bombani, sababu .................
  - . Mtoni, sababu .................
  - . Pengine (taja), sababu .................
- Kutembelea vyoo vya umma (shuleni, zahanati, sokoni, n.k.) na kuona kama vinatosha kulingana na idadi ya watumiaji na hali yake ya usafi (kama hapo juu).
- Kutembelea vituo vya maji kijijini na sehemu nyingine kama sokoni na vituo vya mabasi ili kuona hali ya usafi.

- Andika matokeo ya uchunguzi, kwa mfano:
  . Kuwepo kwa choo 11
  . Sababu ya kutokuwepo choo
    - hakuna mtu wa kujenga 1111
    - hakuna fedha 1
    - choo kilididimia 1111
    - choo kilijaa 111
- Kutoa taarifa ya matokeo katika mkutano wa kijiji (ona hatua ya 4A inayohusu maandalizi ya mkutano).
- Badala ya kuwahutubia, jadili na wanakijiji juu ya mambo yaliyojitokeza.

Mambo ya kuzingatia katika kutoa taarifa ya matokeo hayo:

. Tafuta mawazo ya wanakijiji juu ya mazoea yao ambayo wanadhani yanasababisha kuenea kwa magonjwa kwa njia ya maji.
. Jadili nao juu ya njia za kurekebisha hali ya usafi.
. Jadili nao juu ya mchango wa kila mmoja katika jitihada za kurekebisha hiyo hali.
. Makubaliano yafikiwe kuwa mpango kamili wa utekelezaji utatengenezwa na VWSC, kwa kusaidiana na AFYA.

<u>Hati</u>
Matokeo ya uchunguzi wa hali ya usafi kijijini.

Hatua ya 8B — Elimu ya afya: Majadiliano katika Vikundi

Madhumuni
- Kuinua kiwango cha elimu juu ya uhusiano kati ya maji, usafi wa mazingira na afya.
- Kuhamasisha na kuamsha tabia ya kurekebisha hali ya usafi vijijini.

Washiriki
AFYA, VWSC na watumishi wengine vijijini km VHW, waalimu wa shule na wanakisomo chenye manufaa, viongozi wa wanawake na wa vijana.

Kazi Zitakazofanyika Kijijini
- Kukaa na uongozi wa kijiji na watumishi walioko kijijini na kujadili kila suala katika "Kielelezo cha mafunzo na utendaji".
- Kujadili kwa undani matatizo ya asili kijijini, na njia za asili zinazoweza kutumika kurekebisha hali.
- Kuwaelekeza washiriki kwenda kufanya majadiliano kama hayo katika vikundi vyao.
- Inapobidi, wasaidiwe kuandaa na kupanga kazi zao. Kwa mfano VWSC wanaweza kuwafundisha wajumbe wa nyumba kumi na wake zao elimu ya afya, ili nao wawafundishe majirani zao.

Mambo ya Kufikiria
- Katika kuanzisha majadiliano, anza na mambo ya kawaida yanayotokea kijijini. Kwa mfano, uliza,
  je, vinyesi karibu na sehemu za kuteka maji vitaleta madhara yoyote kiafya? Je kuna haja ya kufanya lolote kuzuia tabia hiyo?

Mwanzoni ilisadikika kwamba kwenda haja ovyo kulikuwa kunaleta madhara kijijini lakini isingedhuru ili mradi kisima kipo mbali na kijiji na kina mfuniko na pampu ya mkono. Pia ilikuwa rahisi kwa watu kutumia vichaka kando ya kisima kwa sababu ya uwezekano wa kupata maji ya kunawa karibu. Majadiliano yagusie wingi wa inzi kuzunguka kisima na jinsi inzi walivyokuwa wanatua na kukaa kwenye vinyesi. Je inzi hawa wangeweza kufika mpaka kijijini na kutua kwenye chakula, na kwenye mikono na nyuso za watoto, na kwa namna hiyo, kusambaza kiasi kkidogo cha kinyesi ambacho kwa bahati mbaya kitamezwa na watu?

Vikundi ambavyo vinaweza kuhusika katika majadiliano na Kamati Ndogo ya Maji/Bwana Afya au Bibi Afya wa Kijiji ni kpamoja na

- Madarasa ya wanafunzi
- Vikundi vya elimu ya watu wazima.
- Vikundi vya akina mama.
- Kundi la majirani (wanapotembeleana majumbani)
- Mikutano iliyoitishwa na wajumbe wa nyumba kumi.

Ni muhimu kuwahusisha wanaume na wanawake katika majadiliano ya vikundi kna katika maamuzi ya vikundi, na kukubaliana kuhusu:

- Ni mambo gani ya uimarishaji wa afya yatafanywa na wanaume na yapi na wanawake.
- Ni majadiliano gani ya vikundi yatafanywa.
- Nani atashiriki na yatahamasishwa vipi (k.m. kuwafahamisha wanawake na wanaume kuhusu mkutano huo na kuufanya wakati ambao ni wa nafasi kwao).
- Nani wataongoza mijadala (mafunzo yao kama lazima).

Baada ya kuundwa kwa vikundi vya majadiliano Kamati Ndogo ya Maji inaweza kuvitembelea kuona ni nani wanashiriki (na kama vikundi vingine haviwezi kukutana), wameamua nini na ni mambo gani wamefanya.

Kumbuka pia: Ni muhimu kufuatilia kazi za Bwana Afya Msaidizi/CDA na kuwapo msaada.

Hatua ya 9 — Kuhamasisha Matumizi ya Maji kwa Ajili ya Kuleta Maendeleo

Madhumuni
- Kuwasaidia VWSC kubuni na kupanga matumizi bora ya maji kwa shughuli za kimaendeleo.
- Kuwasaidia VWSC kubuni na kupanga matumizi ya muda ambao wanawake watakuwa wameokoa kutokana na maji kupatikana karibu.

Washiriki
MAENDELEO, VWSC na wanawake wa kijijini.

Kazi Zitakazofanyika Kijijini
- Kwa kushirikiana na VWSC, MAENDELEO wataangalia kila uwezekano wa matumizi ya maji kwa ajili ya uzalishaji.
  Kati ya matumizi yanayowezekana ni:
  . Kutengeneza matofali ya kujenga majengo ya umma au kuyauza.
  . Bustani ya shule.
  . Bustani ya Zahanati kwa ajili ya maonyesho ya chakula bora.
  . Shunguli za vikundi vya wanawake (bustani, kupikia pombe, ufugaji wa kuku, utengenezaji wa matofali)
  . Vitalu vya miti kwa ajili ya upandaji (kwa mbao, kuni, matunda n.k.)

Mambo ya Kuzingatia
- Mwangalizi wa kisima/Bomba ndiye anayestahili kwanza kutumia maji yanayomwagika nje ya kisima na ya nyongeza na aombwe kutoa ushauri wake wakati wa kuandaa mipango ya matumizi ya maji kwa uzalishaji.
- Faida inayopatikana inaweza kutumiwa kwa uendeshaji na matengenezo ya mradi wa maji.
- Kwa shughuli za wanawake, pata taarifa kutoka kwao juu ya mahitaji yao na yanayowezekana kufanyika.

Hatua ya 10 Matengenezo ya Mradi wa Maji na Gharama Zake

Madhumuni

- Kuelewa umuhimu wa upatikanaji wa maji kwa ustawi wa kijiji.
- Kuwasaidia VWSC katika kukadiria gharama za matengenezo ya mradi kwa mwaka.
- Kuwashauri VWSC katika kukadiria gharama za matengenezo ya mradi kwa mwaka.
- Kuwashauri VWSC juu ya njia zinazoweza kutumika katika kugharamia hayo matengenezo.
- Kuweka utaratibu sahihi wa matengenezo na uangalizi wa maji kijijini.
- Kuwasaidia VWSC katika kuweka utaratibu unaofaa wa utunzaji wa vitabu vya mahesabu.

Washiriki

MAJI, MAENDELEO na VWSC.

Kazi Zitakazofanyika Kijijini

- Kwa kushirikiana na VWSC, fikiria mfano ufuatao:

  "Kijiji cha Loki kimepata kisima kipya. Kila mmoja anafurahi sana. Wanawake hawaendi tena mbali kuteka maji. Sasa wanapata maji mengi zaidi kwa afya bora ya nyumbani na binafsi. Hawachoki kama zamani na wana muda mwingi wa kupika, kuangalia watoto na kilimo. Magonjwa yamepungua kijijini, kwa sababu wanaume, wanawake na watoto wanaweza kuoga na kufua nguo zao mara kwa mara, sasa ni rahisi zaidi kunawa mikono na kuosha vyombo, na kila mmoja anakunywa maji safi. Wanawake wameanzisha bustani za mboga ambazo zinatoa chakula bora zaidi na mapato ya nyongeza. Lakini lo..........usimamizi wa mtambo wa maji ni mbovu. Siku moja unaharibika kabisa na wanawake inawabidi warudie tena kuteka maji kule kwa zamani kwenye maji machafu na ambakoni mbali".

Kutokea nini kijijini na kwa nini?

Fikiria:
. Afya ya kijiji
. Matunzo ya watoto
. Chakula cha familia
. Kazi ya kilimo
. Bustani za mboga
. Shughuli nyingine za kuzalisha fedha
. Mzigo wa kazi kwa wanawake.

Watakaokumbwa zaidi na shida hii kijijini k.m.
. Wazee na vilema
. Wajawazito na wenye watoto
. Wanaonyonyesha
. Watoto wachanga wanaonyonya maziwa ya mama zao.

- MAJI watawasaidia VWSC katika kukadiria gharama za matengenezo kwa mwaka, ikiwa ni pamoja na:
    - . Gharama za vipuli na grisi kwa mwaka.
    - . Gharama za ununuzi wa vifaa vipya.
    - . Malipo ya VM/VSA kwa mwaka.
    - . Gharama za usafiri wakati wa kwenda kununua vipuli na vifaa.
- MAENDELEO watajadiliana na VWSC juu ya njia zitakazofaa zaidi za kupata fedha za matengenezo kijijini.
  Kati ya njia zinazofaa ni:
    - . Kijiji kugharamia kutokana na mapato ya miradi yake, km shamba, duka, mashine ya kusaga, n.k.
    - . Kijiji kugharamia kutokana na mapato mengine ya kijiji km. ushuru wa mazao, ushuru wa soko, n.k.
    - . Kuazisha mfuko maalum wa maji utakaotokana na matumizi ya maji kwa uzalishaji, km kupika pombe, bustani za mboga, kufyatua matofali, n.k.
    - . Michango ya hiari kufikia lengo lililowekwa na VWSC kwa mwaka
    - . Michango ambayo kila kaya itatakiwa kiasi fulani cha fedha kwa mwaka (km baada ya mavuno)
    - . Michango ya mara kwa mara ya kila kaya kijijini.
- MAJI watawafahamisha wanakijiji juu ya ratiba ya ziara ya kufuatilia utekelezaji.
- MAJI wataeleza jinsi ambavyo VWSC itaweza kuwasimamia VM/VSA katika kuweka na kutunza taarifa zinazohusu upatikanaji wa maji na matengenezo ya mradi.
- MAJI watawashauri VWSC juu ya mabadiliko ya bei na utunzaji wa vipuli; vipi vitunzwe kijijini, vipi vitahitajika kwa ajili ya kuchukua nafasi ya vile vinavyoharibika au kuisha na vipuli vipi vinaweza kufanyiwa matengenezo katika karakana.
- MAENDELEO watawashauri VWSC jinsi ya kutunza vitabu vya mahesabu ya fedha za maji.

<u>Mambo ya Kujadili na VWSC</u>

- Utaratibu wa fedha:
    - . Kijiji kina mapato ya kutosha? (angalia akaunti za kijiji)
    - . Je, kijiji kinaweza kuongeza mapato yake? kama ndio, kwa njia gani?
    - . Je, kila kaya inaweza kuchanga kila mwezi, au mapato ni ya msimu?
    - . Ni wakati gani unafaa kukusanya michango?
    - . Unadhani watumiaji wote wa maji wataweza na watakuwa tayari kutoa michango? Kama hapana, utatuzi ni nini?
    - . Unadhani ni vema kila kaya ilipe kiasi kile kile cha fedha wakati matumizi ya maji ni tofauti na uwezo kifedha unaotofautiana? Kama si vema, utaratibu gani utumike? Fikiria kaya zinazonywesha mifugo, kunywesha bustani, wake wengi, vifaa vingi vya kuosha (nguo, magari, nk) kwa upande mmoja na kaya ndogo, maskini wanaoishi mbali na visima/mabomba kwa upande mwingine.

. Je, ni lazima michango iwe ya fedha tu au inaweza kuwa ya vitu? Kama kuna michango ya vitu, itatumika vipi?

- Waulize VWSC uwezekano wa utunzaji mzuri wa vipuli na vifaa. Kwa mwenyekiti wa VWSC. Njia hii itasaidia pia kufuatilia utendaji wa VM/VSA na matumizi ya vipuli.
- Kwa utunzaji mzuri wa fedha za mfuko wa maji, VWSC inaweza kuweka fedha katika akaunti ya kijiji. Ikiwa hivyo, itabidi VWSC waweke taarifa sahihi za mapato na matumizi ya mradi wa maji. Inapendekezwa pia kwamba kwa mapato au matumizi yoyote yale, risiti ziandikwe.
- Uamuzi wa mwisho kuhusu jinsi ya kupata fedha za matengenezo ya mradi uko kwa kijiji chenyewe. Mapendekezo yoyote ya VWSC yatabidi yapitishwe na halmashauri ya kijiji.

<u>Hati</u>

- Ratiba ya ziara ya ufuatiliaji
- Logbook kwa ajili ya VM/VSA
- Vitabu vya mahesabu na akaunti kwa ajili ya VWSC
- Orodha ya bei za vifaa na vipuli

Hatua ya 11 Mafunzo ya VM/VSA na VCT'S

Madhumuni

- Kuwasaidia VWSC kufanya matayarisho ya mafunzo pamoja na VM/VSA na VCT's.
- Kuwasaidia VWSC katika vijiji vyote vitakavyohusika kupanga ushirikiano mzuri wa kuendesha hayo mafunzo.

Washiriki

MAENDELEO na VWSC.

Kazi Zitakazofanyika Kijijini

- Kufahamu ni vitu gani vinatakiwa ili kuwawezesha VM/VSA na VCT's washiriki kwenye mafunzo. Vitu hivyo ni pamoja na posho, msaada wa kutunza nyumba na shamba, n.k.
- Kujadiliana na VWSC na baadhi ya wanawake kijijini jinsi wanawake watakaochaguliwa kwa mafunzo hayo watakavyoweza kuhudhuria. Mambo ya kufikiria ni msaada wa shughuli za shambani, matunzo ya watoto, n.k.
- Majadiliano yafanywe na VWSC's za vijiji vinavyohusika juu ya:
  - Kijiji ambako mafunzo yatafanyika. Ni vizuri kuchagua kijiji chenye mradi, mwamko wa kazi na ikiwezekana kiwe katikati ya vile vingine.
  - Majukumu ya kijiji ambako mafunzo yatafanyika, km. chakula kwa ajili ya wakurufunzi.
  - Michango ya vijiji vingine vitakavyopeleka wakurufunzi, km. chakula, fedha, wapishi, nk.

## Hatua ya 12 Utekelezaji wa Mafunzo ya VM/VSA na VCT's

Madhumuni
- Kuwafunza wanavijiji walioteuliwa kuwa wa kudumu, waendeshaji na watengenezaji wa mradi wa maji katika ngazi ya kijiji.
- Kuwafahamisha VWSC majukumu ya kiufundi ya VM/VSA na VCT's

Washiriki
MAJI, AFYA, MAENDELEO, VM/VSA, VCT's, na VWSC kama wasikilizaji.

Kazi Zitakazofanyika Kijijini
- MAJI watawafunza VM/VSA katika mambo ya kiufundi (angalia kitabu cha mafunzo ya ufundi).
- MAJI watawafunza VCT's juu ya utunzaji wa pampu au bomba na mazingira yake, ujenzi wa mfereji wa maji na jinsi ya kufahamu mapema uharibufu ambao unataka matengenezo.
- MAENDELEO watawafunza VM/VSA, VCT's na VWSC juu ya mawasiliano.
- MAENDELEO na AFYA watawafunza VCT's jinsi ya kuwafunza watumiaji maji matumizi bora.

Mambo ya Kuzingatia
Utunzaji wa vituo vya kuteka maji.

"VCT mmoja katika kijiji cha Sanga Sanga ni mvivu sana. Siku zote utakuta maji yamesimama katika kituo anachotakiwa kutunza. Hii inatokana na sababu nyingi, ikiwa ni pamoja na watoto kuacha maji yakimwagika wa muda mrefu. Kwa sababu hiyo wanyama (ng'ombe, mbuzi, kondoo, nguruwe, n.k.) huja kunywa maji na kuogelea karibu na kituo hicho. Hivi karibuni, mwanakijiji mmoja amejenga choo karibu na kituo hicho cha kuteka maji".

Unadhani ni nini kitawapata wakazi wa Sanga Sanga? Fikiria yale maji machafu, watoto watakaochezea na kunywa hayo maji, mbu, nk.

Mawasiliano
- Kati ya VM na VWSC: Igiza na washiriki hadithi ifuatayo:

"Makanika (au Mhudumu wa Mradi) wa kijiji cha Mamba anatambua sana wajibu wake wa kazi. Daima anahakikisha kwamba maji yanapatikana bila tatizo na kila wakati mwangalizi wa sehemu ya maji anapotoa taarifa ya tatizo, tatizo hilo linashughulikiwa mara iwezekanavyo.

Kijiji kimenunua vifaa na vipuri vyote vya lazima ambavyo vinatunzwa na Makanika/Mhudumu wa Mradi. Ikafika siku ambapo vifaa vyote vikawa vimekwishatumika, mtambo unaharibika na ikawa hakuna maji. Jambo hili lingeweza kuzuilika vipi?

- Kati ya VM na VCT: Igiza na washiriki hadithi ifuatavyo:

  "Ndugu Bomba ni makanika mzuri lakini kamwe hatembelei sehemu za maji mpaka amepata malalamiko. Halafu anakwenda na akikuta matunzo mabaya ya kisima/bomba humkemea Mwangalizi, mama Visima kwa lugha mbaya na kumwaibisha mbele ya majirani na watoto. Mama Visima anajitetea na kunazuka ugomvi. Majirani wanamwunga mkono mama Visima kwa kawaida anaangalia vizuri kisima/bomba. Mtambo unapoharibika tena mama Visima anaogopa kwenda kumtaarifu Ndugu Bomba."

Wakaribishe watu wawili wajifanye kama Ndugu Bomba na Mama Visima wakati wengine wakijifanya ndio majirani.

Jadili namna ambayo, tukio kama hili lingeweza kuzuiliwa.

- Kati ya VCT na VWSC, igiza na washiriki hadithi ifuatayo:

  "Mama Kitambi anapenda sana kazi yake ya utunzaji wa kituo cha kuteka maji. Siku zote anahakikisha kwamba mazingira yake ni safi, na huwaelimisha wanawake wenzake juu ya umuhimu wa maji safi. Siku moja aliona ufa katika sakafu ya kile kituo, na alitoa taarifa kwa VWSC. Aliwaarifu VWSC pia kwamba wanawake wangependa kuwa na mahali pa faragha pa kuoga karibu na kile kituo. Hii itawezesha kuoga na kuwaogesha watoto kila siku. Kwa bahati mbaya VWSC haikuzingatia yale waliyoambiwa na mama Kitambi."

Unadhani ni nini kitatokea?

<u>Kuwaelimisha Wanakijiji Juu ya Matumizi Bora ya Maji</u>
VCT's wafundishwe ili waweze kuaelewesha wanakijiji matumizi bora ya maji katika vituo vyao. Kwanza mwelekeze mwanakijiji mmoja aigize tabia mbaya ya utekaji na matumizi ya maji. Baada ya igizo eleza mambo yanayoweza kutokea kutokana na tabia kama hiyo, kwa mfano:

- Ndoo haioshwi kabla ya kuteka maji.
- Mikono haioshwi.
- Pampu inatumiwa vibaya, au bomba halifungwi.
- Majani yanawekwa kwenye ndoo ili maji yasimwagike.
- Mikono michafu inagusa maji wakati wa kuyabeba.
- Hakuna chombo maalum cha kutunzia maji ya kunywa.
- Chombo chenye maji hakifunikwi.
- Kikombe cha kunywea maji ndicho hicho hicho cha kuchota.

Baada ya hapo, igizo lirudiwe kwa kuonyesha tabia nzuri za utekaji na utunzaji maji. Hizi ni pamoja na:

- . Kusafisha ndoo kabla ya kuteka maji.
- . Kunawa mikono kabla ya kuteka maji.
- . Pampu kutumiwa vizuri na mabomba kufungwa baada ya kuteka maji.
- . Chombo cha maji kufunikwa kwa kifuniko kisafi.
- . Mikono kutogusa maji.
- . Chombo maalum chenye mfuniko kwa ajili ya maji ya kunywa nyumbani.
- . Maji ya kunywa kuchotwa wa kata na kumiminwa kwenye kikombe cha kunywea.
- . Kusuuza kikombe kila baada ya kukitumia.
- . Kuwafundisha watoto tabia hizo nzuri za matumizi ya maji (mtoto anaweza kushirikishwa katika igizo).
- . Maji mengi na sabuni au majivu yatumike kuhakikisha usafi wa mikono baada ya kutoka chooni, kabla ya kupika na kabla ya kula.

Vifaa kwa Igizo:
Ndoo, sabuni au majivu, mtungi wa maji, mfuniko, brashi ya kusugulia au majani yanayotumika kusugulia mitungi, kata yenye mkono mrefu (iliyotengenezwa kwa vifaa vya kienyeji), kikombe cha kunywea maji.

Washiriki
MAENDELEO (Kikosi cha ujenzi pale inapolazimu), VWSC na VCT's.

Kazi Zitakazofanyika Kijijini
- Kukagua na kujadili mpango wa utekelezaji uliotayarishwa na VWSC kuhusu maendeleo.
- Kukagua mafanikio katika kutumia maji kwa uzalishaji.
- Kutoa ushauri na msaada pale penye matatizo.

Hati
Hatua iliyofikiwa katika mpango wa utekelezaji.

## Hatua ya 13 — Kutunga Sheria Ndogo za Matumizi ya Maji na Usafi wa Mazingira

### Madhumuni

- Kuhakikisha kwamba maji safi yanatumika mwaka mazima, angalau kwa kunywa.
- Kuhakikisha kwamba kaya zote kijijini zinajenga vyoo, kuvitunza na kuvitumia.

### Washiriki

AFYA, MAENDELEO na VWSC.

### Kazi Zitakazofanyika Kijijini

- Majadiliano juu ya umuhimu wa sheria ndogo na matumizi yake.
- Majadiliano juu ya yale yatakayokuwemo katika sheria hizo.
- Kupeleka sheria zilizotungwa mbele ya halmashauri ya kijiji ili zipitishwe.

### Mambo ya Kuzingatia

Sheria ndogo ni njia mojawapo ya kuhakikisha kwamba kunakuwa na matumizi bora ya maji safi kijijini na usafi wa mazingira. Hata hivyo, kunaweza kuwepo sababu za msingi za watu fulani fulani kijijini kushindwa kufuata hizo sheria. Mfanoni wakongwe ambao hawawezi kuchimba vyoo, wanakijiji wanaoishi mbali na vituo vya maji safi, ambao wakati wa msimu wa kilimo wataamua kutumia maji yoyote yaliyo karibu, n.k. Ni wajibu wa WVSC kubuni mbinu za kuwasaidia watu wa aina hii. Njia mojawapo ni kwa watoto wa shule kuwasaidia vikongwe kuchimba vyoo na kuvijenga, kubeba maji kwa mikokoteni, n.k.

Hatua ya 14 Kukabidhi Mradi kwa Kijiji

Madhumuni

- Matamshi rasmi ya kijiji kumiliki mradi.
- Kufanya maonyesho ya matumizi bora ya maji na elimu ya afya kwa ujumla kwenye kituo cha kuteka maji.

Washiriki

MAJI, MAENDELEO, AFYA, Serikali ya Kijiji, VWSC, VM/VSA, VCT's na wanakijiji wote.

Kazi Zitakazofanyika Kijijini

- Kurudia maelelzo ya uwajibikaji wa kijiji kwa mradi na manufaa ya kuwepo maji safi kijijini.
- Maelezo juu ya utaratibu wa uendeshaji na matengenezo ya mradi wa maji.
- Kusoma yaliyomo katika hali ya makabidhiano.
- Kutia sahihi hati ya makabidhiano.
- Kufanya maonyesho ya matumizi sahihi ya pampu au bomba, kama yalivyoelezwa kwenye hatua ya 12.

Mambo ya Kuzingatia

Kama kijiji au MAJI hawaridhishwi na jambo lolote katika mradi, hakuna haja ya kukabidhiana mradi. Ihakikishwe kwamba pande zote mbili zimeridhika. Itabidi MAENDELEO wayasikilize kwa makini malalamiko yoyote ya wanakijiji na kuyaeleza kwa wanaohusika.

Hati

Hati ya miliki ya mradi.

## Hatua ya 15 — Mpango wa Kufuatilia Elimu ya Afya na Usafi wa Mazingira

### Madhumuni
- Kuhakikisha kwamba yote yaliyofunzwa, kujadiliwa na kukubaliwa yanatekelezwa.
- Kutatua matatizo au vikwazo vyovyote dhidi ya utekelezaji wa makubaliano.

### Washiriki
AFYA, VHW na VWSC.

### Kazi Zitakazofanyika Kijijini
- Kukagua na kujadili mpango wa utekelezaji uliotayarishwa na VWSC kuhusu maendeleo yatokanayo na maji.
- Kukagua mafanikio.
- Kutoa msaada pale inapolazimu.

### Mambo ya Kuzingatia
Malengo ya kijiji kuhusu elimu ya afya na usafi wa mazingira ni pamoja na:
- Kila kaya kijijini kutumia maji safi wakati wote wa mwaka, angalau kwa kunywa.
- Kwa vijiji vinavyokabiliwa na ugonjwa wa kichocho, maji safi yatumike kwa kufua na kuoga.
- Kuhakikisha usafi wa mazingira katika maeneo ya umma, kama vile mashuleni, mahotelini, sokoni, kwenye zahanati, n.k.
- Watu kutokwenda haja ovyo.
- Kuwepo kwa vyoo visafi, vyenye vifuniko vya mashimo, visivyo na harufu (tumia majivu kupunguza harufu) na vyenye maji na sabuni/majivu kwa ajili ya kunawa mikono.
- Kuelewa jinsi magonjwa yanayoenezwa kwa njia ya maji na mazingira machafu yanavyoambukizwa.
- Pale inapowezekana, vijiji visaidiwe kutumia "slabs" ambazo zinaweza kuhamishwa wakati choo kimoja kinapojaa.
- Katika vijiji vyenye matatizo ya mafuriko au kudidimia kwa vyoo, AFYA watoe ushauri wa kitaalam, kwa mfano kuinua msingi wa choo.

### Hati
Mpango wa kijiji wa utekelezaji.

<u>Hatua ya 16</u> <u>Kufuatilia Matumizi ya Maji kwa Ajili ya Kuleta Maendeleo</u>

<u>Madhumuni</u>

- Kukagua mpango wa utekelezaji uliowekwa kwa ajili ya maendeleo ya kijiji na kuwasaidia VWSC pale inapolazimu.

## Hatua ya 17 Ukaguzi wa Mwaka wa Maji

Madhumuni
- Kukisaidia kijiji katika majukumu ya uendeshaji na matengenezo.

Washiriki
- MAJI, VWSC, VM/VSA na VCT's.

Kazi Zitakazofanyika Kijijini
- Kukagua pampu na mabomba yote kijijini.
- Kukagua visima vyote, na kutia dawa pale inapolazimu.
- Kukagua utendaji kazi wa VM/VSA na VCT's.
- Kutoa mafunzo ya rejea pale inapolazimu.

Hati

Kadi za visima zenye maelezo kuhusu matengenezo, matumizi na hali ya usafi kuzunguka vituo vya kuteka maji.

Hatua ya 18A Tathmini ya Mradi

Madhumuni
- Kutathmini mradi wa maji kijijini.

Washiriki
MAJI, AFYA, MAENDELEO, VWSC, VM/VSA na VCT's, wanakijiji wengine.

Kazi Zitakazofanyika Kijijini
- Kutathmini kazi za VWSC.
- Kutathmini kazi za VM/VSA na VCT's.
- Kutathmini elimu ya afya na utaratibu wa usafi wa mazingira.
- Kutathmini maendeleo yanayotokana na matumizi ya maji kwa uzalishaji.
- Kutathmini kukubalika kwa mradi wa maji kwa wanakijiji.

Mambo ya Kuzingatia
- Ni kwa kipindi gani katika mwaka uliopita maji yalikuwa yanapatikana?
- Je, vituo vyote vya maji vinatunzwa vizuri na pampu kuwekwa grisi?
- Je, wanakijiji wameridhika na huduma hii?
- Je, mfuko wa maji una fedha za kutosha, na zinatunzwa vizuri?
- Je, kila kaya kijijini inatumia maji safi tu, angalau kwa kunywa?
- Ni mpango gani wa elimu ya afya na usafi wa mazingira uliotekelezwa kijijini? Nani walihusika, na kumekuwa na matokeo gani?
- Je, maji yanayomwagika na muda unaookolewa kutokana na maji kupatikana karibu unatumika kwa shughuli gani za maendeleo?
- Je, mradi umeleta shughuli nyingine zozote za kimaendeleo kijijini?

Hati
Taarifa ya tathmini.

## Hatua ya 18B    Uimarishaji wa Vyanzo vya Asili vya Maji Kijijini

Madhumuni
- Kufahamu vijiji ambavyo kwa sababu moja au nyingine haviwezi kupatiwa maji safi ya visima au mabomba, ili vyanzo vya asili vilivyopo vifanyiwe matengenezo na kuimarishwa.
- Kuwasiliana na vyombo vinavyohusika ambavyo vitasaidia katika uimarishaji wa vyanzo hivyo vya asili.
- Kutekeleza uimarishaji wa vyanzo vya asili vya maji kijijini.

Washiriki
MAENDELEO (Kikosi cha Ujenzi), MAJI, AFYA, VWSC, Serikali ya Kijiji na wanakijiji.

Kazi Zitakazofanyika Kijijini
- Wanakijiji wakisaidiana na Kikosi cha Ujenzi watasafisha vyanzo vya asili na kuvijengea pembeni.
- Kuweka nyenzo ya kuchotea maji na kutumia ndoo moja ambayo wakati wote itahakikishwa ni safi.
- Maji kwenye vyanzo hivyo kuwekewa dawa kama zinazowekwa kwenye matanki ya maji ya bomba au kwenye vyanzo.
- Kuvijengea visima vilivyo karibu na mto, ili kuzuia uchafu wakati wa mvua.
- Kutumia mchanga kuchuja maji kwa ajili ya kijiji au watu binafsi.

Mambo ya Kuzingatia
Ili kufahamu jinsi uimarishaji wa vyanzo vya asili utakavyotekelezwa, majadiliano yafanywe na wanakijiji - wanaume na wanawake - ili watoe mawazo yao juu ya njia zitakazofaa kutekeleza kazi hiyo. Msaada mkubwa utaweza kutolewa na Kikosi cha Ujenzi cha Wilaya.

Njia nyingine ya kupata maji safi kwa wakazi wa maeneo kama haya ni kukinga maji ya mvua na kuyatunza. Wakati wa kiangazi mikokoteni ya kukokotwa na wanyama inaweza kutumika kubeba maji safi ambayo yako mbali.

# KUELEWA NA KUIMARISHA HALI YA AFYA YA KIJIJINI

Kielelezo cha Mafunzo na utendaji kwa Wakurufunzi, Waangalizi wa vituo vya maji, Kamati ndogo za Maji za Vijiji na Watumishi wa Afya Vijijini.

SEHEMU YA PILI

Kimetayarishwa na:
PROM/IRC Mradi wa Maendeleo ya Ushirikishaji Jamii Sehemu ya Mpango wa Usambazaji Maji Vijijini Tanzania.

## MAELEZO KWA WATUMIAJI WA KIJITABU HIKI

**Kijitabuhikini kwa ajili ya nani?**

- Waangalizi wa vituo vya maji vijijini na waalimu wao.
- Wale wanakamati wa Kamati ndogo ya maji ya kijiji ambao wana jukumu la kuwaelimisha watumiaji wa visima vya pampu au mabomba.
- Waalimu wanaoishi vijijini na watumishi wa afya.

**Kitabu hiki kina madhumuni gani?**

Madhumuni ya kitabu hiki ni:

- Kuwawezesha waangalizi wa vituo vya maji, wanakamati wa Kamati ndogo na wafanyakazi wa kijiji kuelewa umuhimu wa kutumia maji safi na ya kutosha na wanavijiji wote kuzingatia usafi.
- Kutoa miongozo na vifaa vya elimu (flip charts) ili kusaidia vikundi vidogo vidogo vya wanavijiji katika uimarishaji wa matumizi bora ya maji na tabia ya usafi.

**Jinsi ya kukitumia kitabu hiki wewe mwenyewe**

- fanya mkutano na watumiaji maji kwenye kila kisima/bomba au fanya mikutano ya kirafiki mahali pengine k.m. mikutano ya majirani.
- mwonyeshe kila mmoja kila picha ya kitabu hiki na waulize maswali yaliyomo ndani ya kitabu.
- usitoe majibu yoyote wewe mwenyewe, bali wasaidie watu watoe majibu na mifano yao wenyewe.
- saidia kikundi chako kufanya maamuzi ni jinsi gani watatunza visima/mabomba katika hali ya usafi na kuimarisha matumizi bora ya maji, afya na usafi.


**Watu wengine wanaweza kukitumiaje kitabu hiki?**


Wafanyakazi wa afya wanaweza kukitumia kwa:

- kutembelea watu majumbani kwao na kwa mikutano ya majirani.
- kutembelea sehemu za maji mpya na za kijadi na vyoo vya umma kijijini wakiwa pamoja na kamati ndogo ya maji ya kijiji.
- majadiliano kwenye kliniki.

Waalimu wanaweza kukitumia kwa:-

- Majadiliano katika masomo ya afya darasani.
- majadiliano ya vikundi katika masomo ya elimu ya watu wazima.
- kwa masomo ya vitendo kwa wanafunzi, k.m. kuangalia vyoo vya shule, kutembelea sehemu za maji za kisasa na za kujadi (pamoja na yale yenye vijidudu vya kichocho).





Suala la 1

MAJI MACHAFU HULETA UGONJWA

**Swali:** Maji yaliyo wazi (mto, dimbwi, kisima) yanaweza yakawa na uchafu na vijidudu. Unaweza kutoa mfano jinsi jambo hili linavyoweza kutokea? (Angalia picha)

**Majadiliano:**

- Watu huoga na kufua nguo kwenye mto au kisima. Maji haya baadaye yatanywewa na watu wengine.
- Watu wazima na watoto hujisaidia karibu na maji haya. Mvua hupeleka vinyesi vyao kwenye maji, na mavi ya wanyama pia. Vinyesi hivi vinaweza vikawa na minyoo na vijidudu vibaya. Maji haya yakinywewa, vijidudu na mayai ya minyoo huingia mwilini mwako.

**Swali:**

- Je, maji yaliyo wazi kijijini mwetu hutumika kwa kunywa au kupikia chakula?
- Je, daima maji hayo yanachemshwa hata nyakati za kupanda na kuvuna?
- Ni magonjwa gani unaweza kupata kutokana na kunywa maji yaliyo wazi?

**Jibu:** Magonjwa ambayo watu wanaweza kupata kwa kunywa maji yenye chembechembe za mavi ni kipindupindu, typhoid, (homa ya matumbo) kuhara, kuhara damu na minyoo.

**Swali:** Ni jinsi gani kunywa maji kunaweza kuambukiza wengine magonjwa haya?

**Majadiliano:**

- Watu wazima na watoto ambao wana magonjwa haya (wakati mwingine bila kujitambua) wanaweza kujisaidia karibu na maji.
- Wanaweza kunawa kwenye maji baada ya kujisaidia.
- Nguo zao chafu zinafuliwa kwenye maji hayo.
- Maji haya baadaye yatatumiwa na wengine kwa kunywa na kupikia chakula.
- Watu wazima na watoto wanaokunywa maji haya au kula chakula kilichotayarishwa kwa maji hayo wanaweza kupata magonjwa haya.

**Uamuzi:** Ni maji yapi kijijini mwetu hayana usalama? Kwa nini? Bado utaendelea kuyatumia maji hayo?



Suala la 2 (footpump)

UPATIKANAJI WA MAJI SAFI NI JAMBO ZURI KWA AFYA YA KILA MTU (PAMPU)

Swali: Kwa nini maji kutoka kwenye pampu hayana madhara kwa kunywa?

Majadiliano: Maji kutoka kwenye pampu hutoka chini sana ardhini. Huko hayawezi kuingiliwa na vijidudu vibaya, vinyesi, nguo chafu na miili ya binadamu. Maji haya hupitia bomba refu lililofunikwa mpaka kufika juu (Angalia picha)

Swali: Je, kila mmoja kijijini siku zote atatumia maji kutoka kwenye pampu kwa kunywa na kutayarishia chakula? Unaweza kufikiria wakati ambapo maji yasiyo safi yanaweza kutumiwa?

Majadiliano:


- Pampu iko mbali zaidi kuliko kidimbwi cha karibu, Kisima kisichofunikwa au mto
- Kuna mafoleni kwenye Pampu
- Maji hayana ladha nzuri kulingana na mengine
- Pampu haifanyi kazi vizuri.
- Watoto wetu hucheza karibu na mto au dimbwi na kunywa maji hayo

Swali: Tutahakikisha vipi kwamba kila mtu Kijijini mwetu anakunywa maji safi tu?

Majadiliano:

- Tunaweza kuelekezana sisi wenyewe kuacha kutumia maji yasiyo safi.
- Tunaweza kutunga sheria ndogo ya Kijiji juu ya kutumia maji ya pampu tu.
- Tunaweza kuwaelimisha watoto wetu kuhusu tofauti kati ya maji safi na yenye madhara na kuwaambia wanywe maji kutoka kwenye pampu tu.
- Tunaweza kujitahidi kuzoea ladha tofauti ya maji.
- Tunaweza pia kwenda kuteka maji yetu ya kunywa kutoka kwenye pampu nyingine, kama maji hayo yana ladha nzuri zaidi.
- Tunapokwenda mashambani, tunaweza kuchukua maji safi toka nyumbani.

Uamuzi: Maji kutoka kwenye pampu ni safi kwa sababu Kisima kimefunikwa na kuzuia uchafu. Maji hayo pia yamechunguzwa na mafundi wa MAJI ili kuhakikisha kwamba ni salama kuyanywa, hata kama yana ladha tofauti kidogo. Tutumie maji safi tu kwa kunywa na kupikia.



Suala la 2 (handpump)

UPATIKANAJI WA MAJI SAFI NI JAMBO ZURI KWA AFYA YA KILA MTU (PAMPU)

Swali: Kwa nini maji kutoka kwenye pampu hayana madhara kwa kunywa?

Majadiliano: Maji kutoka kwenye pampu hutoka chini sana ardhini. Huko hayawezi kuingiliwa na vijidudu vibaya, vinyesi, nguo chafu na miili ya binadamu. Maji haya hupitia bomba refu lililofunikwa mpaka kufika juu (Angalia picha)

Swali: Je, kila mmoja kijijini siku zote atatumia maji kutoka kwenye pampu kwa kunywa na kutayarishia chakula? Unaweza kufikiria wakati ambapo maji yasiyo safi yanaweza kutumiwa?

Majadiliano:


- Pampu iko mbali zaidi kuliko kidimbwi cha karibu, Kisima kisichofunikwa au mto.
- Kuna mafoleni kwenye Pampu.
- Maji hayana ladha nzuri kulingana na mengine.
- Pampu haifanyi kazi vizuri.
- Watoto wetu hucheza karibu na mto au dimbwi na kunywa maji hayo.

Swali: Tutahakikisha vipi kwamba kila mtu Kijijini mwetu anakunywa maji safi tu?

Majadiliano:

- Tunaweza kuelekezana sisi wenyewe kuacha kutumia maji ya pampu tu.
- Tunaweza kuwaelimisha watoto wetu kuhusu tofauti kati ya maji safi na yenye madhara na kuwaambia wanywe maji kutoka kwenye pampu tu.
- Tunaweza kujitahidi kuzoea ladha tofauti ya maji.
- Tunaweza pia kwenda kuteka maji yetu ya kunywa kutoka kwenye pampu nyingine, kama maji hayo yana ladha nzuri zaidi.
- Tunapokwenda mashambani, tunaweza kuchukua maji safi toka nyumbani.

Uamuzi: Maji katika pampu ni safi kwa sababu Kisima kimefunikwa na kuzuia uchafu. Maji hayo pia yamechunguzwa na mafundi wa MAJI ili kuhakikisha kwamba ni salama kuyanywa, hata kama yana ladha tofauti kidogo. Tutumie maji safi tu kwa kunywa na kupikia.



Suala la 2 (Mabomba)

UPATIKANAJI WA MAJI SAFI NI JAMBO ZURI KWA AFYA YA KILA MTU(MABOMBA)

**Swali:** Kwa nini maji kutoka kwenye bomba hayana madhara kuyanywa?

**Majadiliano:**

- Kwenye vijiji vyenye maji ya kuchimbwa: Maji kutoka kwenye mabomba yanatoka chini sana ardhini. Huko hayawezi kuchafuliwa na vijidudu vibaya kutoka kwenye vinyesi vya watu, wanyama wala nguo chafu.
- Katika Vijiji ambavyo hupata maji kutoka kwenye mabomba yanayokinga maji milimani: Maji hutoka katika sehemu ya mto ambako hakuna watu wanaoishi. Kwa hiyo maji hayawezi kuchafuliwa na watu wanaonawa au kuoga mtoni wala vinyesi ambavyo huingizwa kwenye maji na mvua.

**Swali:** Je, kila mmoja kijijini atatumia maji ya bomba kwa kunywa? Unaweza kufikiria nyakati ambazo maji yaliyo wazi yatatumika badala ya maji ya bomba?

**Majadiliano:**

- Bomba lililo karibu kabisa lipo mbali zaidi kuliko kisima cha wazi au maji mengine yaliyo wazi ambayo yanaweza kuwa machafu.
- Kuna mafoleni bombani.
- Maji hayapatikani nyakati zile zile siku zote.
- Bomba limeharibika.
- Kuna maji mengi na tope kuzunguka bomba.
- Watoto hucheza karibu na mto na kunywa maji huko.

**Swali:** Tutahakikishaje kwamba ni maji safi tu yanatumika kwa kunywa kijijini mwetu?

**Majadiliano:**

- Tunaweza kuelekezana sisi wenyewe kuacha kutumia maji yasiyo safi.
- Tunaweza kutunga sheria ndogo ya kijiji kukataza matumizi ya maji yasiyo safi kwa kunywa.
- Tunaweza kuiambia kamati ya maji ibadilishe nyakati za uendeshaji au wahakikishe kwamba bomba linatengenezwa mara linapoharibika.
- Tunaweza kuwaelimisha watoto wetu juu ya tofauti kati ya maji safi na yenye madhara na kuwaambia wanywe maji kutoka kwenye bomba tu.
- Tutakwenda na maji safi shuleni, shambani, n.k.

**Uamuzi:** Maji ya bomba hayatadhuru afya yetu kama yanatoka mahali ambako hakuna anayeweza kuyachafua. Kila mmoja kijijini mwetu, wanaume, wanawake na watoto wanywe maji safi tu.



Suala la 3 (Footpumps)

JE, MAJI SAFI YANAKUWA SAFI DAIMA? (PAMPU)

Swali: Maji, yaliyo chini ya ardhi yamekingwa yasichafuliwe na watu au wanyama. Ni nini kinaweza kutokea kama maji machafu yanakusanyika kuzunguka pampu?

Majadiliano: Maji machafu yanaweza kuzama ardhini na kuchafua maji safi yanayovutwa juu. Jambo hili linaweza kutokea kwa pampu ya miguu au ya mkono.


Swali: Ni nini kinaweza kutokea kama mfuniko wa Kisima una nyufa au umeondolewa?


Majadiliano: Uchafu utaingia na wanyama (panya) watatumbukia Ndoo chafu na kamba zake zinaweza kuleta vijidudu vibaya kwenye maji, kama zitatumbukizwa.

Swali: Tunawezaje kuzuia maji kisimani chini ya pampu yasichafuliwe?

Majadiliano:
- Kila mtumiaji ahakikishe kwamba mfereji ni safi na maji hayajikusanyi kuzunguka pampu.
- Kama ni lazima, mfereji uchimbwe kuondoa maji yanayomwagika. Migomba, Miwa, mboga za majani au karo mwishoni mwa mfereji vitasaidiana kunyonya maji machafu.
- Nyua za miti au waya zijengwe kuzunguka pampu. Wanyama wasiruhusiwe ndani ya nyua.
- Vyoo visijengwe chini ya meta 20 kutoka kwenye pampu. Mtu yoyote asitumie eneo la pampu kama choo.
- Kuoga na kufua nguo kufanywe mbali na pampu na maji yamwagwe kwenye mfereji.
- Wakati fulani kunaweza kukahitajika vifaa maalum kwa kufulia na kuogea, k.m. vijiji vyenye kichocho au watu wengi hufua na kuoga kwenye pampu. Mambo ya kujadili ni:
  - . Wapi vinahitajika
  - . Vitalipiwa vipi
  - . Watumiaji (wanawake) wanataka viwe namna gani
  - . Nani ataviangalia
- Mifuniko yenye nyufa inatengenezwa na waangalizi wa visima wakisaidiwa na kijiji (Kamati ndogo ya maji)
- Pampu ikiharibika, kisima kisifunuliwe bali pampu itengenezwe upesi.

Uamuzi: Kuyatunza maji yetu ya kunywa katika hali ya usafi, tuweke mazingira ya pampu katika hali ya usafi na wanyama wasiruhusiwe humo. Waangalizi na Kamati ndogo waone kwamba visima vinatunzwa vizuri.





Suala la 3 (Handpumps)

JE, MAJI SAFI YANAKUWA SAFI DAIMA? (PAMPU)

Swali: Maji yaliyo chini ya ardhi yamekingwa yasichafuliwe na watu au wanyama. Ni nini kinaweza kutokea kama maji machafu yanakusanyika kuzunguka pampu?

Majadiliano: Maji machafu yanaweza kuzama ardhini na kuchafua maji safi yanayovutwa juu. Jambo hili linaweza kutokea kwa pampu ya moguu au ya mkono.

Swali: Ni nini kinaweza kutokea kama mfuniko wa Kisima una nyufa au umeondolewa?

Majadiliano: Uchafu utaingia na wanyama (panya) watatumbukia. Ndoo chafu na kamba zake zinaweza kuleta vijidudu vibaya kwenye maji, kama zitatumbukizwa.

Swali: Tutawezaje kuzuia maji kisimani chini ya kpampu yasichafuliwe?

Majadiliano:
- Kila mtumiaji ahakikishe kwamba mfereji ni safi na maji hayajikusanyi kuzunguka pampu.
- Kama ni lazima, mfereji uchimbwe kuondoa maji yanayomwagika. Migomba, Miwa, Mboga za Majani au karo mwishoni mwa mfereji vitasaidia kunyonya maji machafu.
- Nyua za miti au waya zijengwe kuzunguka pampu. Wanyama wasiruhusiwe ndani ya nyua.
- Vyoo visijengwe chini ya meta 20 kutoka kwenye pampu. Mtu yeyote asitumie eneo la pampu kama choo.
- Kuoga na kufua nguo kufanywe mbali na pampu na maji yamwagwe kwenye mfereji.
- Wakati fulani kunaweza kukahitajika vifaa maalum kwa kufulia na kuogea, k.m. vijiji vyenye kichocho au watu wengi hufua na kuoga kwenye pampu. Mambo ya kujadili ni:
  . Wapi vinahitajika
  . Vitalipiwa vipi
  . Watumiaji (wanawake) wanataka viwe namna gani
  . Nani ataviangalia
- Mifuniko yenye nyufa inatengenezwa na waangalizi wa visima wakisaidiwa na kijiji (Kamati ndogo ya maji)
- Pampu ikiharibika, kisima kisifunuliwe bali pampu itengenezwe upesi.

Uamuzi: Kuyatunza maji yetu ya kunywa katika hali ya usafi, tuweke mazingira ya pampu katika hali ya usafi na wanyama wasiruhusiwe humo. Waangalizi na Kamati ndogo waone kwamba visima vinatunzwa vizuri.

Suala la 3 (mabomba)

JE, MAJI SAFI YANAKUWA SAFI DAIMA? (MABOMBA)

Swali: Mahali ambapo maji huingia kwenye mabomba huitwa "intake". Panaweza pakawa kwenye mto. Je, maji kutoka kwenye mabomba yatakuwa bado safi kama maji kwenye "intake" yamechafuliwa? Maji kwenye "intake" yanaweza kuchafuliwa namna gani?

Majadiliano:

- Wanyama (k.m. ng'ombe) wanakunywa maji juu ya "intake". Vinyesi vyao vinaingia kwenye mto na kufukia mahali maji yanapoingia kwenye mabomba.
- Watu wanakuja kuishi au kulima karibu na "intake". Hawatumii vyoo ila vichaka karibu na mto.
- Watu wanafua na kuoga karibu na "intake", watoto hucheza na kuogelea. Vinyesi vyao vinaingia majini.

Swali: Tufanye nini ili "intake" iwe katika hali ya usafi?


Majadiliano:

- Hakikisha kwamba ng'ombe hawaruhusiwe karibu na mto. Tengeneza mahali pa kunyweshea ng'ombe chini ya "intake".
- Jadili na wakulima juu ya usafi wa maji karibu na "intake". Washauri wafue nguo na kuoga sehemu ambazo ni chini ya "intake", watumie vyoo na kufukia vinyesi wanapokuwa mashambani.
- Waelimishe watoto waogelee chini ya "intake" na kufukia vinyesi vyote au watumie vyoo.
- Chemsha maji yote ya kunywa (angalau kwa watoto wadogo) kama hakuna uhakika wa usafi wa maji ya bomba. Waombe watu wa MAJI wachunguze maji hayo na kifanywe nini kama maji si safi tena.

Swali: Ni nini kinaweza kutokea kama maji yanakusanyika kwenye valvu au mabomba? (Valvu hutumika kusafishia mabomba mara kwa mara).

Majadiliano: Kama mabomba hayana maji, maji machafu yanaweza kupenya kwenye vitundu na nyufa za bomba na kuingia ndani.

Uamuzi: Maji ya bomba ni safi tu pale maji hayo yanapotoka sehemu iliyo safi. Kwa hiyo tuhakikishe kwamba hakuna uchafu au maji machafu yanayoweza kuingia katika mabomba kwenye "intake", valvu au mabomba yanakotumika. Tukidhani kwamba maji ya bomba si safi tena, tuchemshe maji yetu ya kunywa na kuwaomba watu wa MAJI ushauri:



Suala la 4

MBU HUZALIANA KWENYE MAJI YALIYOSIMAMA

Swali: Kwa nini ni vibaya pia kuwa na maji yaliyosimama katika mazingira ya pampu au mabomba? (Angalia picha)

Majadiliano: Mbu huzaliana kwenye maji yaliyosimama. Wanaweza kueneza malaria, matende na homa ya manjano kwa kumuuma kwanza mtu aliye na ugonjwa na halafu kuwauma watu wasio na ugonjwa. (Minyoo ya safura pia hupenda sehemu za unyevunyevu. Jambo hili lijadiliwe chini ya suala la 12).

Swali: Ni wapi maji yanaweza kukusanyika kijijini mwetu?

Majadiliano:

- Kuzunguka visima au mabomba (madimbwi)
- Madimbwi ya mvua kijijini na katika barabara za kijiji.
- Katika makopo ya zamani yaliyotupwa, vibuyu, mitaro, mashimo kwenye miti na mimea kuzunguka nyumba.
- Kwenye matenki ya kuhifadhia maji na mapipa ambayo hayakufunikwa.
- Kwenye sehemu za kuogea na kufulia.

KUMBUKA: Hasa, ni katika sehemu za ukame ambako uwekaji wa pampu au mabomba unaweza kuongeza malaria na magonjwa mengine yanayoletwa na mbu. Hii ni kwa sababu kuwepo kwa maji yanayosimama huleta huko sehemu mpya za mbu kuzaliana ambazo hazikuwepo kabla.

Uamuzi: Ili kupunguza sehemu ambazo mbu wanaweza kuzaliana, kwa kiasi kikubwa inavyowezekana, kusiwepo na maji yanayosimama kwenye pampu na visima, pasiwe na makopo ya zamani, mapipa ya maji yasiyofunikwa, mitaro na mabwawa karibu na nyumba. Inapowezekana, maji yanayosimama yakaushwe kwa kuchimba mifereji na njia za mifereji zitengenezwe kutoka barabarani.



Suala la 5 (pampu)

KUHARIBIKA KWA PAMPU NA AFYA YA KIJIJI (PAMPU)

**Swali:** Kwa muda fulani kijiji kimekuwa na maji ya kutosha na safi kwa kunywa. Sasa mojawapo ya pampu inaharibika. Watumaiji wa pampu hiyo hawaendi kwenye pampu nyingine, lakini wanarudia kutumia maji yaliyo wazi. Matumbo yao yamezoea maji safi. Nini kinaweza kuzipata familia kijijini? Na watoto wao?

**Majadiliano:** Kwanza tumbo lako limezoea maji safi. Ghafla unapata maji yenye vijidudu kutoka kwenye vinyesi vya watu wengine, unapatwa na ugonjwa kirahisi. Watoto wadogo hasa hupatwa na ugonjwa mara kwa mara kuliko watoto wakubwa na watu wazima.

**Swali:** Tunaweza kufanya nini ili kulinda afya ya familia zetu kama pampu inaharibika?


**Majadiliano:**

- Tusifunue kisima ila tujaribu kutengeneza pampu haraka iwezekanavyo kwa msaada wa makanika wa kijiji wa kijiji na Kamati ndogo ya maji ya kijiji.
- Kama makanika wa kijiji anashindwa kutengeneza tuombe msaada kutoka nje ya kijiji.

**Swali:** Tunawezaje kufahamu kama pampu yetu inafanya kazi vizuri?

- Chunguza kama pampu imekaa imara kwenye kikalio chake.
- Angalia kama kuna sehemu zozote zilizolegea (nati, Parafujo, mkono wa kushikia).
- Kwa pampu ya mkono: jaribu kupampu kwa kirefu na kikamilifu. Kwa namna hii pampu itakuwa na maisha marefu zaidi.
- Wafundishe watoto jinsi ya kupampu vizuri. Watoto wasiruhusiwe kuchezea pampu. Wanaweza kuelezwa kwa nini pampu ni muhimu, na kuwahamasisha wacheze michezo mingine.

**Uamuzi:** Tutumie pampu vizuri ili ziendelee kufanya kazi. Kama kuna matatizo, tumfahamishe makanika. Tutumie pampu nyingine au tuchemshe maji ya kunywa mpaka pampu imetengenezwa. Tuiombe Kamati ndogo ya maji ya kijiji yafanywe matengenezo ya haraka.



Suala la 5 (mabomba)

KUKOSEKANA KWA MAJI YA MABOMBA

Swali: Kijiji kimekuwa na maji ya kutosha kwa muda fulani. Sasa baadhi ya mabomba yameharibika. Au mfumo mzima wa kupata maji kwa mabomba umeharibika. Watu wanarudi kuteka maji kwenye visima vyao vya zamani. Baadhi ya visima hivi vimechafuliwa kwa vinyesi. Matumbo ya watu yamezoea maji safi. Nini kitawapata watu na watoto wanaokunywa maji haya machafu?


Majadiliano: Kama tumbo limezoea kwanza maji safi halafu linapata maji machafu unaweza kupata ugonjwa upesi sana. Watoto wadogo hasa hupatwa na ugonjwa wa kuhara zaidi kuliko watoto wakubwa na watu wazima.

Swali: Tufanye nini ili kulinda afya ya familia zetu kama hakuna maji kwenye mojawapo ya mabomba?

Majadiliano:

- Tunakwenda kwenye bomba lingine kuchota maji ya kunywa. Kama bomba hili lipo mbali sana au kama hakuna bomba lingine ambalo linafanya kazi, angalau kwa watoto wadogo.
- Tumwarifu mwangalizi/makanika mara tuonapo kwamba kuna tatizo. Pengine mabomba yanaweza kutengenezwa kabla mfumo mzima haujaharibika kabisa.
- Wakati mwingine watu wanaoishi au kutembea kando ya njia za mabomba wanaweza kuona kasoro fulani (bomba linalovuja au lililopasuka, "intake" iliyoziba). Wanaweza kumwarifu mwangalizi.
- Tuwaombe makanika na Kamati ndogo wafanye matengenezo ya haraka. Kama makanika hawezi kufanya matengenezo, tuombe msaada kutoka nje ya kijiji.

Uamuzi: Tutumie mabomba vizuri ili yaendelee kufanya kazi. Kama kuna matatizo, tumjulishe mwangalizi. Kama bomba au mfumo mzima wa mabomba unaharibika tuchemshe maji ya kunywa, angalau kwa watoto wadogo. Tuiombe Kamati ndogo ya maji ya kijiji ifanye matengenezo ya haraka.



Suala la 6

UCHOTAJI WA MAJI YA KUNYWA BILA KULETA MADHARA

Swali: Maji safi kutoka kwenye pampu au bomba hayaleti madhara kwa afya ya watu. Lakini maji haya si lazima yawe safi siku zote. Yanawezaje kuchafuliwa wakati wa kuyachota? (Angalia picha)

Majadiliano:


- Watu wazima na watoto wanabeba maji kwenye mitungi isiyooshwa au ndoo chafu.
- Wanaweka majani juu ya mitungi au ndoo ili kuzuia maji yasimwagike. Majani haya yanaweza yakawa machafu.
- Maji yaliyomo kwenye mitungi au ndoo yanaguswa na mikono michafu wakati wa kuyapeleka nyumbani.

Swali: Tunaweza kufanya nini ili kuhakikisha kwamba maji safi kutoka kwenye pampu au bomba hayachafuliwi?

Majadiliano:

- Osha mikono, mitungi na ndoo kabla ya kuchota maji.
- Funika mtungi kwa mfuniko ulio safi kuzuia maji yasimwagike.
- Jiepushe na ugusaji maji wakati wa kuyapeleka nyumbani.
- Waonyeshe watoto jinsi ya kuchota maji inavyotakiwa.

Uamuzi: Ili maji yetu yaliyo safi yaendelee kuwa safi tuoshe mikono yetu, mitungi na ndoo kabla ya kuyachota. Tutumie mifuniko safi kuzuia maji yasimwagike. Tusiyaguse maji hayo. Tuwafundishe watoto wetu jinsi ya kuchota maji kwa namna inayotakiwa. Tujadili na watumiaji wengine uchotaji maji kwa namna ambayo haitaleta madhara.



Suala la 7

UTUNZAJI NA UCHOTAJI WA MAJI YA KUNYWA NYUMBANI

Swali: Je, ni kwa njia zipi maji safi kutoka kwenye pampu au bomba yanaweza kutunzwa kwa usalama ili kuepukana na madhara?

Majadiliano:
- Tumia mtungi maalum kwa kutunzia maji ya kunywa.
- Safisha mtungi huo kabla ya kuujaza maji mapya.
- Safisha mtungi wa maji ya kunywa mara kwa mara kwa sabuni au mchanga ili kuhakikisha kwamba umekuwa safi kabisa.
- Funika mtungi daima.

Swali: Je, maji kutoka kwenye mtungi wa kutunzia maji yanawezaje kuchafuliwa wakati wa kuyachota?


Majadiliano: Mikono michafu (k.m. baada ya kutoka chooni) inaweza kuchafua maji kwa kuyagusa. Watoto pia wanapochota maji kwa mikono yao, au wanapochota maji kwa chombo cha kunywea.

Swali: Tunawezaje kujiepusha na kugusa maji tunapoyachota kutoka kwenye mtungi?

Majadiliano:
- Mimina maji bila kuyagusa.
- Tumia kata yenye mkono mrefu (k.m. ya kibuyu au kopo) kuchotea maji ili kuyaweka kwenye mtungi mwingine au kikombe (Angalia picha)
- Mfundishe kila mmoja ndani ya nyumba jinsi ya kuchota maji kutoka kwenye mtungi wa kutunzia maji ya kunywa. Waeleze watoto kwa nini wasichovye mikono yao au vikombe vyao kwenye mtungi huo.

Kumbuka: Bwana Afya, mwangalizi, Kamati ndogo ya maji au mwalimu wanaweza kuandaa kielelezo cha njia nzuri na mbaya za uchotaji maji bombani, utunzaji wake na uchotaji wa maji ya kunywa nyumbani.

Uamuzi: Tutunze maji yetu ya kunywa katika chombo cha pekee, kilicho safi na kufunikwa. Tutumie Kata yenye mkono mrefu au tumimine maji. Tusiyaguse maji. Tuwafundishe watoto wetu jinsi ya kutumia kata.



Suala la 8

TUMIA MAJI MENGI ZAIDI KWA KUFULIA NA KUOGA

Swali: Ni magonjwa gani unaweza kuyapata kama hutumii maji mara kwa mara, kwa kuosha mikono yako, nguo na vyombo vya jikoni, kuosha watoto wako (hasa mikono yao na nyuso zao) na kuosha uso wako mwenyewe na mwili?

Majadiliano:

- Magonjwa ya tumbo, kama chakula kinatayarishwa na kuliwa kwa mikono isiyooshwa, au kutumia vyombo vichafu.
- Magonjwa ya macho, kwa sababu macho ambayo hayaoshwi mara kwa mara wakati wa kiangazi kudhurika kwa vumbi na inzi. Kama macho yameambukiwa na ugonjwa, yaoshe mara kwa mara kwa maji ya chumvi. Tumia kitambaa safi kujikaushia.
- Magonjwa ya ngozi, na homa itokanayo na vidudu vinavyokaa mwilini k.m. chawa. Magonjwa haya huambukiwa kwa vidudu hivi vinavyokaa kwenye ngozi, nguo na nguo za Kitandani. Kama unapata ugonjwa wa ngozi, tumia brashi na sabuni kufulia nguo na nguo za Kitandani mara kwa mara. Kuoga na kufua nguo mara kwa mara kunaweza kuzüia kupata ugonjwa na kuponyesha aina hii ya ugonjwa wa ngozi.

Swali: Tunaweza kufanya nini ili tupunguze uwezekano wa kupata magonjwa haya? (Angalia picha)

Majadiliano:

- Tuoshe mikono yetu mara kwa mara, kwa sabuni kama inawezekana.
- Tuoshe mikono ya watoto, nyuso na miili yao mara kwa mara.
- Tuoshe vyombo vya kupikia na kulia kila siku na tuvikaushe kwenye kichanja juani (Angalia picha).
- Jadiliana na Kamati ndogo ya maji na watu wa MAJI kujenga sehemu ya kufulia na kuogea karibu na bomba/pampu.


Uamuzi: Kwa afya bora, ni muhimu kwamba tutumie maji mengi zaidi kwa kuogea mara kwa mara sisi wenyewe na watoto wetu (hasa mikono), nguo zetu, nguo za Kitandani na vyombo vya jikoni.



Suala la 9

CHOO BORA KWA KILA MTU

| | |
|---|---|
| Swali: | Baadhi ya watu hawatumii vyoo kwa sababu hawakujenga, au kwa sababu vyoo hivyo siyo vizuri kuvitumia. Je, unafahamu matatizo yoyote yale kuhusu vyoo katika familia yako au kwa majirani? |
| Majadiliano: | - Kuna hatari ya vyoo kubomoka, kudidimia kwa vyoo havina paa na mvua huingia.<br>- Vinanuka vibaya.<br>- Baadhi ya familia hazina mtu wa kuwasaidia kuchimba choo (k.m. wazee, wanawake wasioolewa na wana watoto wadogo)<br>- Baadhi ya wanaume hawapendi kutumia vyoo au kushirikiana na watoto wao wa kike.<br>- Wanaume wengine hawataki kujenga choo kipya au kusaidia kuimarisha kile cha zamani. |
| Swali: | Tufanye nini ili kujaribu kutatua matatizo haya? |
| Majadiliano: | - Imarisha sakafu ya choo (miti imara, kuchanganya majivu, mavi ya ng'ombe pamoja na udongo. Kuweka sakafu ya saruji inapowezekana.<br>- Imarisha shimo kwa vifaa vinavyopatikana hapo (k.m. matofali ya kuchoma. Paka mafuta ya oil chafu kwenye mbao au miti ili kuzuia mchwa).<br>- Chimba mashimo mawili ya vyoo kwenye kibanda kimoja au viwili kwa wanaume na kingine kwa wanawake.<br>- Toa ushauri kwa majirani ambao hawana choo juu ya uchimbaji na ujengaji wa vyoo.<br>- Andaa misaada ya kuwachimbia na kuwajengea vyoo familia ambazo hazina watu wenye nguvu au wavulana wakubwa.<br>- Waombe msaada watu wa AFYA katika matatizo magumu (k.m. ardhi tifutifu). |
| Uamuzi: | Kwa afya bora ya kijiji, kila familia kijijini inapaswa kuwa na choo kizuri na kukitumia. Tuwasaidie wale ambao hawana choo kujenga chao. |



Suala la 10

CHOO SAFI NI AFYA PIA

Swali:

Kama watu wakinywa maji yenye chembechembe za kinyesi, wanaweza kupata magonjwa ya tumbo (kuhara, kipindupindu, typhoid (homa za matumbo), minyoo n.k. lakini zipo njia zingine ambazo unaweza ukameza kinyesi kwa bahati mbaya. Unaweza kufikiria mfano?

Majadiliano:

- Choo cha nyumbani au shuleni ni kichafu. Inzi hutua kwenye uchafu halafu hutua kwenye chakula.
- Mikono haioshwi baada ya kwenda chooni. Chakula kinatayarishwa au kuliwa kwa mikono michafu.
- Watoto wadogo wanatambaa kwenye kiwanja ambapo vinyesi vimetapakaa. Wanashika vinyesi halafu wanalamba vidole vyao.
- Vinyesi havichimbiwi kijijini au karibu na maji. Inzi hutua kwenye kinyesi halafu hutua kwenye chakula.
- Watu hujisaidia chini ya miti ya matunda. Matunda yanadondoka. Yanaokotwa na kuliwa bila kuonshwa.

Swali:


Tufanye nini ili kuepukana na uwezekano wote wa kumeza chembechembe za vinyesi?

Majadiliano:

- Kamwe kusiwe na vinyesi vilivyoachwa bila kufukiwa, hata mavi ya watoto (angalia picha).
- Vyoo vyote vitunzwe katika hali ya usafi na tumia mfuniko wa kuzuia inzi kwenye shimo wenye mkono mrefu.
- Weka maji sabuni ya kuoshea mikono ndani ya, au karibu na choo.
- Watoto wetu wafundishwe kutumia choo siku zote na kunawa mikono baada ya haja.
- Hakikisha kwamba kuna vyoo vya kutosha na safi shuleni, (na maji na sabuni ya kunawia mikono).
- Itungwe sheria itakayokataza kuwepo kwa vinyesi visivyofunikwa au kuchimbiwa katika eneo la kijiji, kuzunguka visima, karibu na kituo cha basi n.k.
- Maporini: chimba shimo na fukia kinyesi kwa udongo.

Uamuzi:

Kwa afya bora ya kijiji, siyo tunywe maji safi tu, bali tujiepushe na kumeza chembechembe za vinyesi kwa njia zingine, kama vile kwa mikono michafu, vyoo vichafu, inzi na vyombo vichafu vya jikoni.



Suala la 11

NI MUHIMU KUNAWA MIKONO VIZURI

**Swali:** Kwa nini ni muhimu kunawa mikono kwa sabuni?


**Majadiliano:** Mikono michafu inaweza kuleta madhara kwenye maji na chakula. Chakula hiki kikiliwa au maji haya kunywewa, unaweza ukaugua. Watoto wadogo nao mara kwa mara hunyonya vidole vyao na kwa namna hii humeza vijidudu. Maji na sabuni husafisha mikono vizuri zaidi kuliko maji peke yake. Kama hatuna sabuni, tunaweza kutumia mchanga, majivu au majani.

**Swali:** Wakati gani ni muhimu kunawa mikono?

**Majadiliano:**

- Wakati wa kuchota maji ya kunywa
- Baada ya kwenda haja (watoto pia) nyumbani na kwingineko.
- Baada ya kuwapangusa choo watoto wachanga na wadogo.
- Kabla ya kula.

**Uamuzi:** Ni muhimu kunawa mikono kwa sabuni baada ya kwenda haja na kabla ya kuchota maji na kutayarisha chakula. Kama hatuna sabuni, tutumie mchanga, majivu. Kwa namna hii tutahakikisha kwamba tumeondoa vijidudu na mayai ya minyoo kwenye mikono yetu. Tuwafundishe watoto wetu kufanya hivyo hivyo.



Suala la 12

SAFURA

Swali: Watu wa kijijini wanapata ugonjwa wa Safura? Unawezaje kupata ugonjwa huu?

Majadiliano: Mtu mwenye Safura anakwenda haja kivulini kwenye kichaka. Mayai ya minyoo ya Safura hutoka nje. Mayai huanguliwa katika sehemu ya unyevunyevu kivulini. Minyoo mipya hungoja mpaka mtu mwingine apitae sehemu hiyo na kuingia kwenye nyayo zake. Inatambaa mpaka kufikia tumboni mwake. Humo wanaanza kutaga mayai mapya ambayo yatatoka nje kwa njia ya kinyesi cha mtu huyu. Mayai yanaanguliwa na watu wengi zaidi watapata minyoo ya safura.

Swali: Tufanye nini ili kuzuia kuambukizwa Safura? (Angalia picha).

Majadiliano:

- Kusiwe na vinyesi ambavyo havikuchimbiwa kuzunguka kijiji na kijijini penyewe.
- Kusiwe na vinyesi karibu na pampu au mabomba au kwenye kituo cha basi.
- Chimbia kinyesi kwenye shimo lenye kina kirefu sehemu kavu kama unafanya kazi shambani au porini.
- Vaa viatu au makubazi hasa wakati wa mvua au kwenye sehemu za unyevunyevu.
- Pata matibabu ukiwa na Safura na uwe mwangalifu sana katika kutumia choo bila kukichafua. Kama mayai yote yanaangukia chooni yatakufa.

Uamuzi: Kuzuia uenezaji wa Safura, kila mmoja kijijini mwetu (wanaume, wanawake na watoto) inambidi atumie vyoo, na kuchimbia kinyesi sehemu kavu ikiwa wapo shambani au porini. Kuvaa viatu au makubazi kutazuia minyoo ya Safura kuingia kwenye nyayo zetu.



Suala la 13

KICHOCHO

Swali:

- Je, kuna kichocho kijijini?
- Watu wanapataje ugonjwa huu? (Angalia picha).


Majadiliano: Watu wazima na watoto ambao wana kichocho wana minyoo midogo tumboni mwao. Mayai ya minyoo hii hutoka nje kwa njia ya mkojo wao au kinyesi. Kama watu wanakojoa au kwenda haja kwenye maji au karibu na maji, mayai huwaingia konokono wa kichocho ambao wanaishi ndani au karibu na maji hayo. Ndani ya konokono mayai haya hutotoa na kuwa minyoo. Minyoo hiyo huwaacha konokono na kutafuta mtu aliyesimama au kuogelea kwenye maji hayo. Wanapenya ngozi ya mtu huyo na kufikia tumboni mwake. Humo wanaanza kutaga mayai. Mayai hutoka nje katika mkojo au kinyesi na pengine kuambukiza watu wengine wapya. Baada ya muda fulani watu zaidi na zaidi watapata minyoo hii.

Swali: Tunaweza kufanya nini ili kuzuia ugonjwa huu kuenea kwa wengine?

Majadiliano:

- Mtu yoyote yule asikojoe au kwenda haja karibu na au ndani ya maji yaliyo wazi k.m. Kisima kisichofunikwa, mto, n.k.
- Kama inajulikana kwamba maji ya kijijini au yaliyo karibu na kijiji yana kichocho, watu wajue kwamba ni hatari kuoga, kufua au kuogelea kwenye maji hayo. Ukitumia muda mrefu zaidi kwenye maji haya, basi uwezekano wa kupata minyoo mingi ya kichocho mwilini mwako ni mkubwa zaidi.
- Inapowezekana, sehemu zingine za usalama ziwekwe kwa ajili ya kuogea na kufulia nguo n.k. sehemu maalum ya kufulia na kibanda cha kuogea karibu na pampu au bomba la maji safi.
- Wanaume, wanawake na watoto wanaojihisi wana kichocho (damu kwenye mkojo au kinyesi) waende Zahanati kwa matibabu. Wawe waangalifu sana wasijisaidie kwenye au karibu na maji. Chooni, mayai ya minyoo hayawezi kutotoa kwa sababu hakuna konokono ambamo yanaweza kukulia. Kwa hiyo, mayai ya kichocho yatakufa chooni bila kuwa minyoo.

Uamuzi: Mtu yoyote yule asiende haja kwenye, au karibu na maji. Watu wajiepushe kuoga, kufua nguo au kuogelea kwenye maji yenye minyoo ya kichocho. Minyoo hiyo inaweza kukuingia kupitia ngozi yako ukikaa hata kwa muda mfupi kwenye maji hayo.



Suala la 14

## JINSI YA KUTIBU UGONJWA WA KUHARA KWA WATOTO

**Swali:**

- Je, kuhara ni tatizo la kiafya kijijini kwako?
- Unadhani ni haki tuwe na wasiwasi juu ya ugonjwa huu?

**Majadiliano:**

Kuhara kunasababisha maji ya mwilini mwa mtoto kukauka. Ukaukaji wa maji mwilini husababisha vifo vya watoto wengi Tanzania. Imekadiriwa kwamba kuhara ni ugonjwa wa tatu kwa kusababisha vifo na pengine ndio ugonjwa wa mara kwa mara kuliko mwingine wowote kwa watoto Tanzania. Uchunguzi unaonyesha kwamba idadi kubwa ya watoto kufikia 50-60,000 wanakufa kwa ugonjwa wa kuhara kila mwaka.

**Swali:**

Tufanye nini ili kuzuia ukaukaji wa maji kwenye miili ya watoto?

**Majadiliano:**

- Kama mtoto wako anahara, unaweza kuzuia au kutibu ukaukaji wa maji kwa kumpa mtoto mgonjwa mchanganyiko wa maji na chumvi.
- Mchoto mmoja wa chumvi kwa vidole vitatu na mchoto mmoja wa sukari kwa mkono na kuyeyusha kwenye nusu lita ya maji safi ya kunywa (tumia chupa moja ya bia kama kipimo) ni njia nzuri ya kuzuia au kutibu ukaukaji wa maji mwilini.
- Mtoto anaweza kupewa maji hayo hata kufukia kiasi cha lita mbili (chupa nne za bia) kama anahara.
- Mtoto anywe maji haya ya mchanganyiko wa chumvi na sukari kwa kutumia kikombe au kijiko na kwa kiasi ambacho atakubali kunywa kwa wakati mmoja.

**Uamuzi:**

Mtoto abembelezwe ale kama kawaida hata kama anahara. Kama hali ya mtoto inazidi kuwa mbaya, pamoja na kunywa maji haya, au kama hawezi kunywa kabisa, basi apelekwe Zahanati kwa matibabu zaidi.

